BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**FEBRUARI, 2022**

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**YALIOMO**

SEHEMU YA KWANZA ....- 4-

1. UTANGULIZI .... - 1 -

*1.1* UTARATIBU NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI .... - 2 -

*1.2* KUPITIA MISWADA YA SHERIA .... - 3 -

*1.3* MUUNDO WA KAMATI .... - 3 -

*1.4* HADIDU REJEA .... - 4 -

SEHEMU YA PILI .... - 5 -

2.0 OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA .... - 5 -

2.1 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA OR, UTUMISHI NA UTAWALA BORA .... - 6 -

2.2 MAHAKAMA KUU .... - 6 -

2.3 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA .... - 8 -

2.4 AFISI YA MWANASHERIA MKUU .... - 10 -

2.5 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR .... - 11 -

2.6 IDARA YA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA .... - 13 -

2.7 UANZISHWAJI WA SKULI YA SHERIA ZANZIBAR .... - 13 -

2.8 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR .... - 14 -

2.9 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI .... - 16 -

2.10 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA .... - 18 -

2.11 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO .... - 18 -

2.12 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR – ZAECA .... - 20 -

2.13 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI .... - 21 -

3.0 OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ .... - 23 -

3.1 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ ....- 24 -

3.2 JESHI LA KUJENGA UCHUMI *(JKU)* .... - 24 -

3.3 WAKALA WA ULINZI WA JKU: .... - 24 -

3.4 CHUO CHA MAFUNZO (MF) .... - 27 -

3.5 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) .... - 29 -

**3.6 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)** - 31 -

**3.7 KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ)** - 33 -

**3.8 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI** - 34 -

**3.9 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR** - 36 -

**3.10 BARAZA LA MANISPAA MJINI** - 38 -

**3.11 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A"** - 41 -

**3.12 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"** - 42 -

**3.13 OFISI YA MKOA WA KUSINI UNGUJA** - 46 -

**3.14 BARAZA LA MJI KATI** - 47 -

**3.15 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA** - 48 -

**3.16 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA** - 49 -

**3.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI "A"** - 50 -

**3.18 BARAZA LA MJI KASKAZINI "B"** - 52 -

**3.19 OFISI YA MKOA WA KUSINI PEMBA** - 54 -

**3.20 OFISI YA MKUU WA MKOA KUSINI PEMBA.** - 55 -

**3.21 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE.** - 56 -

**3.22 BARAZA LA MJI MKOANI-PEMBA.** - 58 -

**3.23 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI PEMBA** - 59 -

**3.24 OFISI YA MKUU WA WILAYA WETE** - 62 -

**3.25 OFISI YA MKUU WA WILAYA MICHEWENI - 63 -**

**3.26 BARAZA LA MJI WETE - 65 -**

**3.26 HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI - 67 -**

**3.27 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** - 69 -

**4.0 OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS** - 72 -

**5.0 OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI** - 80 -

**5.1 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS** - 80 -

**5.2 BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR** - 80 -

**5.3 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR** - 81 -

**5.4 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (III)** - 81 -

**SEHEMU YA TATU** - 84 -

**6.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA JUMLA YA KAMATI** - 84 -

# SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambayo imeundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha *85* cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* na Kanuni ya *107(1)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka *2020*.

Ripoti hii inaakisi kazi zote za Kamati ambazo zimefanywa kuhusiana na utekelezaji wa Taasisi ambazo zipo chini yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha, 2021/2022 na kwa kuzingatia Mipango mikuu ya Kitaifa ambayo inajumuisha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Chama Chama Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025. Aidha, majukumu ya Kamati hii, yameelezwa katika *Jadweli la Kwanza* la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kama ifuatavyo:

(i) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.
(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
(iv) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
(v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati hii ni ya Kisekta ambayo inasimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara *nne (4)* zifuatazo:

*(a)* Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

(b) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum.
(c) Ofisi ya Makamu wa Kwanza Rais.
(d) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

## *1.1* UTARATIBU NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Katika sehemu hii Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeelezea utaratibu wa kazi zake zilizofanywa na Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka 2020 kwa kupokea taarifa tofauti za kila robo mwaka (quarterly reports) za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara, kupokea taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati pamoja na kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kutoa ushauri wa kutatua changamoto zilizojitokeza kwa Taasisi mbali mbali za Kiserikali pamoja na kazi ya kupitia Miswada ya Sheria.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ilitekeleza kazi zake kwa kusimamia malengo yafuatayo:

*(a)* Kufuatilia maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka *2019/2020*.
*(b)* Kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka wa fedha *2021/2022*.
*(c)* Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka wa fedha *2021/2022*.
*(d)* Kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika Taasisi za Serikali pamoja na kufanya ziara katika Taasisi husika.

Kwa mwaka wa fedha *2020/2021* na *2021/2022*, Kamati ilifanya kazi zake za mizunguuko mitatu (3) kwa muda wa wiki Kumi na Moja *(11)* katika utaratibu ufuatao:

*(i)* Kuanzia tarehe *18 Januari, 2021* hadi *29 Januari, 2021*, Kamati ilitekeleza majukumu yake Unguja.
*(ii)* Kuanzia tarehe *29 Machi, 2021* hadi *10 Aprili, 2021*, Kamati ilitekeleza majukumu yake Unguja na Pemba.
*(iii)* Kuanzia tarehe *09 Agosti, 2021* hadi *20 Agosti, 2021*, Kamati ilitekeleza majukumu yake Unguja na Pemba. Pia, kuanzia

tarehe *23 Agosti 2021* hadi *28 Agosti 2021* Kamati ilitekeleza majukumu yake Tanzania Bara.

*(iv)* Kuanzia tarehe *08 Novemba, 2021* hadi *26 Novemba, 2021* ambapo Kamati ilitekeleza majukumu yake Unguja na Pemba.

*(v)* Kuanzia tarehe *17 Januari, 2022* hadi *04 Februari, 2022* ambapo Kamati ilitekeleza majukumu yake Kisiwani Pemba, Tanzania Bara na Unguja.

## *1.2* KUPITIA MISWADA YA SHERIA

Katika majukumu ya msingi ya Kamati pia imepewa nafasi ya kushughulikia Miswada ya Sheria ambayo itapelekwa na Spika. Kwa kipindi hiki, Kamati iliweza kupitia Miswada ifuatayo:-

*(a)* Mswada wa Marekebisho Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake, 2021.

*(b)* Mswada wa Kuanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Kuweka Usimamizi Bora wa Shughuli za Kiislam Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

*(c)* Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani yake, *2021*.

*(d)* Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti, Nam. *9* ya *2001*.

*(e)* Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kazi, Majukumu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

*(f)* Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake.

## *1.3* MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaundwa na Wajumbe wafuatao:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *9.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *10.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

## *1.4* HADIDU REJEA

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kutekeleza majukumu yake ilitumia:

*(a)* Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984*.
*(b)* Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka *2020*.
*(c)* Ripoti ya Kamati ya mwaka 2019/2020.
*(d)* Hotuba za Bajeti kwa mwaka wa fedha *2020/*2021 na *2021/2022* za Wizara zifuatazo:

- *(i)* *Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora*;
- *(ii)* *Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ;*
- *(iii)* *Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;*
- *(iv)* *Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais*

*(e)* Taarifa za Utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi husika.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia masuala ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Ofisi ina jumla ya Idara na Taasisi 11 zinazosimamiwa na Katibu Mkuu na Taasisi 4 zinazopokea Ruzuku kutoka Serikalini. Idara na Taasisi hizo ni ni kama zifuatazo:-

*(i)* Idara ya Utumishi na Uendeshaji.
*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(iii)* Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.
*(iv)* Wakala wa Serikali Mtandao.
*(v)* Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu.
*(vi)* Idara ya Msaada wa Kisheria.
*(vii)* Idara ya Utawala Bora.
*(viii)* Ofisi ya Mufti.
*(ix)* Afisi Kuu Pemba.

Aidha, Taasisi 4 zinapokea ruzuku kutoka Serikalini ili kutekeleza majukumu yake kama zilivyopangiwa. Taasisi hizo ni kama zifuatavyo:-

*(i)* Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.
*(ii)* Chuo cha Utumishi wa Umma *(IPA)*.
*(iii)* Ofisi ya Mufti.
*(iv)* Ofisi ya Waqfu na Mali ya Amana.

Vile vile, Wizara hii inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

*(i)* Mahkama Kuu.
*(ii)* Afisi ya Mwanasheria Mkuu.
*(iii)* Mkurugenzi wa Mashtaka
*(iv)* Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
*(v)* Tume ya Kurekebisha Sheria.
*(vi)* Afisi ya Rais Baraza la Mapinduzi.
*(vii)* Kamisheni ya Utumishi wa Umma.
*(viii)* Tume ya Utumishi Serikalini.
*(ix)* Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

## 2.1 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Katika Sehemu hii ya Sekta ya Sheria inahusisha Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa haki, Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria, Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai, Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria na Programu ya Usimamizi wa Masuala ya dini. Programu hizi zinatekelezwa kupitia Mahkama Kuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofisi ya Mufti, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Idara ya Msaada wa Kisheria.

## 2.2 MAHAKAMA KUU

Mahakama Kuu Zanzibar ina jukumu la kutafsiri sheria, kusikiliza kesi na kutoa uamuzi kufuatana na sheria za nchi. Vile vile, Mahakama ina jukumu la kusikiliza na kutoa uamuzi wa kesi zote zinazohusiana na masuala ya jinai na madai. Katika kipindi cha Julai – Septemba 2021, Kamati imeweza kufuatilia kwa kina utekelezaji wa Taasisi zinazojishughulisha na usimamizi wa haki katika jamii. Katika kipindi hiki Kamati imebaini kwamba Mahkama imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

*(i)* Jumla ya kesi za jinai 2,503 zilifunguliwa katika Mahkama mbali mbali na kesi 1,810 zimetolewa uamuzi. Kati ya kesi hizo, kesi 191 za udhalilishaji zilifunguliwa na kesi 14 zimetolewa uamuzi;

*(ii)* Jumla ya kesi za madai 718 zilifunguliwa na kesi 120 zimetolewa uamuzi, Kesi 20 zimefunguliwa katika mahkama ya kazi na kesi 1 imetolewa uamuzi;

*(iii)* Kufanya kikao cha Kamati ya Kusukuma kesi (Case Flow Management Committee). Kikao kilijadili utaratibu wa kuwapeleka na kuwarejesha Mahakamani Wanafunzi na Mahabusu; changamoto ya Wakemia kutokuhudhuria Mahakamani kwa ajili ya kuthibitisha uchunguzi walioufanya; Polisi kutokuheshimu amri za Mahkama katika maombi ya "Habeas corpus"; utaratibu wa kufanyakazi baada ya saa za kazi; Vituo vya mkono kwa mkono na Dhamana kwa makosa ya udhalilishaji.

**CHANGAMOTO ZA MAHKAMA KUU ZANZIBAR:**

*(a)* Kamati imesikitishwa na suala la uchakavu wa majengo ya Mahakama na vitendea kazi vyao ambapo Kamati haikuridhishwa na namna ya nyaraka zinavohifadhiwa katika Mahakama.

*(b)* Kamati imebaini kwamba katika taratibu za kisheria Zanzibar inaruhusika Mahkama kutoa adhabu ya kuitumikia jamii kwa wahalifu lakini bado mpaka leo sheria hii haijatekelezwa n ahivyo kusababisha mrundikano mkubwa wa wanafunzi katika Chuo cha Mafunzo.

*(c)* Uhaba wa fedha za matumizi mengineyo ambapo hupelekea ugumu wa baadhi ya majukumu na manung'uniko kwa jamii kutokana na kushindwa kulipwa stahiki zao kama vile nauli kwa mashahidi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(a)* Mahakama zimetakiwa kufanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida jambo ambalo ni gumu kutekelezeka, hivyo, tunashauri Serikali kuandaa mradi maalum wa kuyafanyia matengenezo majengo yote ya Mahakama kwa Unguja na Pemba.

*(b)* Kamati inashauri kulipwa kwa malimbikizo ya madeni ya fedha za mashahidi ili kutowakatisha tamaa mashahidi hao ambao ni muhimu katika upatikanaji wa haki.

*(c)* Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu maalum wa kuhakikisha Mahakama ya Watoto Pemba, inakuwa na miundombinu itakayowawezesha watoto wenye ulemavu kuhudumiwa katika Mahakama kwa urahisi zaidi.

*(d)* Kufuatia Kamati kutoridhika na utaratibu unaotumiwa katika Mahakama za Watoto Kisiwani Pemba kwa kutoa hukumu ya faini tu kwa watoto kwa makosa mbali mbali kutokana na ukosefu wa Gereza la watoto Kisiwani Pemba.Hivyo,Kamati inashauri kutafuta mbinu mbadala za kuweza kutafuta sehemu ya Chuo cha Mafunzo cha Watoto ili na wao wapate kujifunza tabia njema.

## 2.3 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar ndio yenye dhamana ya kuziendesha kesi zote za jinai hapa Zanzibar. Katika utekelezaji wake, Taasisi hii imefanikiwa katika mabo yafuatayo:-

*(i)* Kuendesha kesi 859 katika mahakama mbali mbali za Unguja na Pemba katika kipindi kifupi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti yake. Ambapo kati ya kesi 181 ni kesi za udhalilishaji, 103 ni kesi za madawa ya kulevya na 575 zinahusiana na makosa mengineyo.

*(ii)* Kusimamia na kuendesha kesi 181 zilizofunguliwa katika Mahakama maalumu za udhalilishaji. Kati ya hizo, kesi 54 zimepata hatia, kesi 40 zimeachiwa huru, kesi 11 zimeondolewa na Mahkama na tisa (9) zimeondolewa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

*(iii)* Kamati imeridhishwa na kuongezeka kwa idadi ya mashahidi wanaojitokeza kutoa ushahidi katika kesi za jinai na kuwapatia ushauri wa kisheria unaostahiki ili kurahisisha uendeshaji wa kesi. Jumla ya Mashahidi 534 walipokelewa kutokana na muamko wa wananchi katika kutoa ushahidi na kufuatilia kesi za udhalilishaji kwa kipindi cha july/septemba, 2021.

*(iv)* Kufanya mkutano wa mwaka wa wahusika wa haki jinai kwa ajili ya kujadili changamoto zinazojitokeza katika uendeshaji wa kesi za jinai ikiwemo kesi za udhalilishaji na kuzipatia ufumbuzi wa kufaa.

*(v)* Kuwapatia mafunzo watumishi wapya 18 wa kada za sheria na utawala ili kuwawezesha kufanya kazi kwa uweledi.

*(vi)* Aidha, Kamati imeridhika na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti (ZLRC) Zanzibar kutokana na mwamko mzuri wa wanafunzi katika fani za sheria.

*(vii)* Kituo kimeweza kutunukiwa ithibati kamili yaani "*full accreditation*" kutoka baraza la taifa la elimu ya ufundi (NACTE) tarehe 25.06.2021. Kabla ya kutunukiwa ithibati hiyo, kituo kilikua kina usajili (full registration) kutoka NACTE.

**CHANGAMOTO OFISI YA MKURUGENZI WA MASHATAKA ZANZIBAR:**

*(a)* Ukosefu wa majengo ya ofisi na madarasa ya kufundishia kwa kituo cha sheria Zanzibar;

*(b)* Kusitishwa kwa udahili wa wanafunzi kwa muhula wa mwezi wa machi, 2021 kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ambako kumepelekea kituo kukosa mapato yatokanayo na makusanyo ya ada ya wanafunzi;

*(c)* Kukosekana na kwa wanafunzi wa kutosha wa kushirikia mafunzo ya muda mfupi; na

*(d)* Ukosefu wa usafiri, tatizo ambalo limeshafanyiwa kazi kwa kuwekwa katika bajeti ya kituo kwa mwaka 2021/2022. Pamoja na uchakavu wa gari mbili za Afisi ya Pemba hali inayopelekea kuzifanyia matengenezo mara kwa mara ili kuweza kutekeleza majukumu ya kiafisi.

*(e)* Mashahidi wenye umri kati ya miaka 15 hadi 17 kwenye makosa ya udhalilishaji wanawake kukataa kutoa ushahidi wa mtindo mpya wa kutowatambua washtakiwa wakiwa mahakamani.

*(f)* Kukoa Afisi ya kudumu kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba ambapo kwa sasa jengo linalotumika ni la kukodi.

*(g)* Upungufu wa watumishi katika kada mbalimbali kwa upande wa Pemba hali inayopelekea kuomba watumishi kutoka taasisi nyengine kwa njia ya uhamisho wa kuazimwa au uhamisho wa moja kwa moja.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(a)* Kamati inashauri kituo kuzidi kusimamia upatikanaji wa majengo yake kwa kukusanya mapato kwa uhakika pamoja na kutafuta wafadhili ambao watasaidia katika ujenzi wao;

*(b)* Kamati inashauri kituo kwenda samabamba na mitaala ya kitaifa na kimataifa ili kutoa wanafunzi bora ambao watahudumu katika sekta za sheria kwa nchi zote za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati;

*(c)* Kamati pia, inashauri kituo kujitangaza katika vyanzo mbali mbali vya habari ili jamii ya wanafunzi na watumishi wa umma

watambue uwepo wa kituo hiki hapa Zanzibar pamoja na umuhimu wake katika sekta ya sheria.

*(d)* Kamati inashauri kutafuta mbinu mbadala za kuelimisha jamii juu ya dhana nzima ya utoaji ushahidi kwa vijana wenye umri wa miaka 15 mpaka 17 kwa kuwatumia viongozi wa dini na wasanii na hata mitandao ya kijamii.

*(e)* Kamati pia inashauri Wizara kuwafikiria kwa kuwapatia jengo jengine Kisiwani Pemba litaloendana na wakati na kuepuka kupoteza gharama nyingi wanazotumia kwa ajili ya kukodi Afisi.

*(f)* Kamati inaiomba Serikali na Wizara kulitafutia ufumbuzi suala la kuajiri wafanyakazi wataokidhi vigezo vya kuwa waendesha Mashtaka.

## 2.4 AFISI YA MWANASHERIA MKUU

Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, ambapo kwa kipindi hiki imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

*(i)* Kuimarisha mfumo wa Sheria za Zanzibar na kuandaa Kanuni Nane (8) zinazotokana na Sheria tofauti kwa lengo la kuzifanya Sheria hizo ziweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi;

*(ii)* Kuandaa Matangazo ya Kisheria 58 kuhusu mambo mbali mbali yaliohitaji kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali;

*(iii)* Kufanya mapitio ya Rasimu za Mikataba 178 na kutoa ushauri, kati ya hiyo, rasimu za Mikataba 103 inahusiana na ununuzi wa bidhaa na huduma, rasimu za mikataba 20 ya ujenzi, 18 zinahusiana na Ushauri elekezi na 18 inahusiana namasuala ya kodi;

*(iv)* Kufanya mapitio ya Hati za Maelewano (MoU) 19 zilipitiwa na kutolewa ushauri kwa Wizara naTaasisi mbalimbali za Serikali;

*(v)* Kuendelea kuiwakilisha Serikali kwenye mashauri ya Kesi za madai na kutoa ushauri wa Kisheria kuhusiana na mashauri hayo;

*(vi)* Kusimamia kesi 89 kwa Unguja na Pemba, kati ya hizo, kesi 11 mpya zilisajiliwa na kesi saba (3) zimefikia hatua ya kutolewa uamuzi.

**CHANGAMOTO ZA AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR:**

*(a)* Uhaba wa wafanyakazi wa kada mbalimbali kwa Unguja na Pemba.

*(b)* Uchelewaji wa Mikaataba kutokana na Mikataba hiyo kukosa kupitiwa ipasavyo na Taasisi husika kabla kufikishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

*(c)* Kuchelewa kupelekwa kwa Mikataba katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na kuhimizwa kuitoa kwa haraka.

*(d)* Uhaba wafedha za matumizi mengineyo hali inayopelekea kukwama kwa baadhi ya majukumu.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(a)* Kamati inashauri kuwe na utaratibu maalumu wa kupitia mikataba kabla ya kuifikisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

*(b)* Kamati inaiomba Serikali na Wizara kuwapatiakibali cha uajiri hali itayosaidia kufanyakazi kwa ufanisi zaidi.

*(c)* Kamati inaishauri Afisi kutoa elimu zaidi kwa wananchi juu ya umuhimu wa kupata mafunzo kupitia mradi wa Uwezeshaji wa Sekta ya Sheriana upatikanaji haki (LEAP).

## 2.5 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imeanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria Namba 16 ya Mwaka1086. Katika kuimarisha sekta ya sheria nchini, Serikali imeendelea kuzifanyia mapitio sheria mbalimbali za Zanzibar ambazo zimeonekana kuwa na changamoto katika utekelezaji wake, sheria hizo ni kama vile:-

*(i)* Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya Mwaka 2011; Mapitio ya eneo linalohitaji uanzishwaji wa Taasisi ya Wahasibu Wakaguzi wa Hesabu na Washauri wa Kodi; Mapitio ya Eneo linalohitajika usimamizi wa Sekta ndogo za Fedha (Microfinance); Mapitio ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Namba 16 ya Mwaka 1986; Mapitio ya Sheria ya Madawa ya Kulevya ambayo imeshakamilika na kupitishwa rasmi katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Mapitio ya Sheria ya Mufti; Mapitio ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Afisi ya Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na Mapitio ya Sheria ya kuanzishwa kwa Jumuiya Zanzibar.

*(ii)* Kukamilisha ripoti ya ukusanyaji maoni katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) hasa katika eneo la kikokotoo cha Mafao ya Wastaafu; Eneo la Migogoro ya Ardhi na Utatuzi wake; Eneo la Ndoa na Talaka; Sheria ya Uvuvi na uhifadhi wa Bahari; Sheria ya Kazi; Sheria ya Mkonga wa Taifa (e – Government); Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; Sheria ya Leseni za Biashara; na Sheria ya Mazingira.

*(iii)* Kutafsiri Sheria ya Umiliki wa Ardhi (Land Tenure Act) kwa lugha nyepesi.

*(iv)* Kuanzisha kipindi maalumu cha Televisheni kinachorushwa hewani na ZBC siku ya Jumatatu kuanzia 3:30 hadi saa 4:45.

**CHANGAMOTO ZA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA:**

1. Uelewa mdogo wa Jamii kuhusu masuala ya Sheria pamoja na kutofahamika kwa Tume ya kurekebisha Sheria na majukumu yake kwa Jamii,
2. Kuwepo kwa Sheria nyingi zenye mapungufu na zinazohitaji kufanyiwa marekebisho.
3. Kutokuwepo mazingira bora ya kufanyia kazi kunakosababisha nauchakavu wa Jengo,ufinyu wa ofisi na uhaba wa vyombo vya usafiri,
4. Uhaba wa fedha za matumizi kwa mujibu wa bajeti iliyowasilishwa.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaishauri Serikali kuipatia Tume Jengo linaloendana na hadhi yao ambalo litakidhi haja ya wafanyakazi.
2. Kamati inashauri Tume kuzifanyia mapitio sheriazote zenye kuleta ugumu wa utekelezaji wake badalayakusubiri kuletewa.
3. Kamati inashauri baadhi ya Taasisi ambazo huzipeleka sheria zao kufanyi wa mapitio na baadae wanashindwa kuziendeleza sheria hizo.
4. Kamati inaishauri Serikali na Wizara kuwapatia mafunzo wafanyakazi wao japo ya nchi jirani ili kuongeza ujuzi wa kazi zao.

## 2.6 IDARA YA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA

Program ya kutoa huduma za msaada wa kisheria inasimamiwa na Idara ya Huduma za Kisheria ikiwa na lengo kuisadia jamii juu ya masuala ya kisheria. Hivyo, kupitia ziara mbali mbali za Kamati imeelezwa kwamba Idara imeweza kutekeleza mambo yafutayo:-

*(i)* Kuandaa Rasimu ya Muongozo wa Uratibu wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa watoa huduma 40wakiwemo Maafisa Sheria wa Halmashauri, Polisi, Wenyekiti wa Masheha na Taasisi za watoa huduma za msaada wa kisheria.

*(ii)* Kutoa elimu kwa umma kuhusu upatikanaji wa msaada wa kisheria, masuala ya udhalilishaji na nafasi ya Watoa huduma za msaada wa kisheria katika jamii kupitia vipindi vya saba (7) vya televisheni na redio.

*(iii)* Kuchapisha na kusambaza nakala 100 za Kanuni za Malipo ya Wakili na Vakili kwa wahusika wa msaada wa kisheria kama vile, Mahakama, Jumuiya ya Mawakili Zanzibar na Taasisi za Watoa huduma za Msaada wa Kisheria;

*(iv)* Kupokea na kutatua malalamiko matatu (3) ya wananchi. Kati ya hayo mawili (2) yanahusu kazi na 1 linahusu fidia.

*(v)* Kuwafikia wananchi 337 (wanawake 272 na wanaume 65) wa Shehia nne za Unguja ambazo ni Mbuzini, Bwejuu, Fuoni Migombnai na Fujoni kwa kuwasikiliza malalamiko yao ya kisheria na kuwapatia elimu ya sheria kuhusu udhalilishaji na migogoro ya ardhi.

**CHANGAMOTO ZA IDARA YA MSAADA WA KISHERIA:**

Uhaba wa Wasaidizi wa Sheria katika baadhi ya Shehia za Unguja na Pemba.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Kamati inashauri kuharakisha utoaji wa mafunzo ya elimu ya usaidizi wa sheria kwa wanafunzi ambao wanatoka ndani ya majimbo kwa ajili ya kuongeza idadi ya watoa huduma za msaada wa kisheria.

## 2.7 UANZISHWAJI WA SKULI YA SHERIA ZANZIBAR

Programu hii inasimamiwa na Skuli ya Sheria Zanzibar ambapo imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa uwazi

zaidi katika kujenga mustakbali bora wa fani ya sheria nchini. Katika kipindi cha miezi mitatu ya July – Septemba, 2021 skuli imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

*(a)* Kutayarisha michoro ya ujenzi wa jengo la ghorofa mbili na majengo mengine madogo ya Skuli ya Sheria yatakayo jengwa Tunguu, nyuma ya jengo jipya la Mahakama, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja;

*(b)* Kutayarisha Kanuni za Skuli ya Sheria na kuwasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa hatua zaidi. Kanuni zenyewe ni Kanuni ya Udhibiti wa Tabia ya Wanafunzi na Kanuni za Taaluma, Ada na Mafunzo ya Vitendo.

*(c)* Matayarisho ya Mitaala ya Skuli ya Sheria yanaendelea kupitia Mradi wa LEAP; Kwa sasa, Skuli ya Sheria imeruhusiwa kutumia Mtaala wa Skuli ya Sheria ya Tanzania bila ya malipo. Kutokana na kutokuwepo Mtaala, Skuli ya Sheria Zanzibar imeomba kutumia Mtaala wa masomo ya vitendo ya Sheria;

*(d)* Kuanzisha udahili wa wanafunzi wanaojiunga na chuo kwa njia ya matandao (online admission system) Mfumo wa mtandao huo utaiwezesha Skuli kutambua uhalali wa vyeti vyao. Kwa sasa, zoezi la udahili linaendelea na wanafunzi wameanza kuomba kujiunga na Skuli ya Sheria ya Zanzibar.

## 2.8 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR

Kamati imeridhishwa sana na utekelezaji wa majukumu ya taasisi hii pamoja na taasisi ya Muft Zanzibar ambazo ndio kioo cha masuala ya dini ya Kiislamu hapa nchini. Aidha, katika utekelezaji wa programu hii Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ndani ya miezi mitatu imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

*(a)* Kutoa fatwa 227 na ufafanuzi wa masuala na miongozo mbalimbali ya kidini kuhusu ndoa, talaka, mirathi, kuslimu, kupotea kwa watu na mambo mengine ya kifamilia.

*(b)* Kupokea na kutatua migogoro 103 ya ndoa, talaka na masuala mengine ya kijamii. Kati ya migogoro hiyo, 64 inahusu ndoa na talaka na migogoro 39 inahusu masuala ya mirathi, malezi ya watoto, wasia na huduma za kifamilia.

*(c)* Jumla ya tirka 287 (242 Unguja na 45 kwa Pemba) zimefungwa na warithi kupatiwa haki zao sawa na 61% ya shabaha.

*(d)* Jumla ya mali zenye thamani ya Shilingi 12,311,834,518.13 (Unguja 11,443,676,024.83 na 868,158,493.30 Pemba) zimerithishwa kwa wananchi;

*(e)* Kamisheni imeweza kusimamia kesi mbali mbali kupitia Mahakama Kuu na Mahakama ya Kadhi katika ngazi tofauti;

*(f)* Mizozo 25 (7 Unguja na 18 Pemba) imeshughulikiwa, 13 imepatiwa ufumbuzi na mizozo 12 inaendelea kutafutiwa ufumbuzi na mashauri 45 yamepatiwa ushauri wa kisheria (25 Unguja na 20 Pemba) sawa na 125% ya makadirio. Jumla ya Mikataba 45 imepitiwa na kutolewa (44 ya upangishaji 1 wa ujenzi); na

*(g)* Kuratibu ugawaji wa sadaka ya fedha taslim Shilingi 32,400,000 iliyotolewa na Jumuiya ya One Ummah kwa mayatima 120 wenye umri chini ya miaka 16 kwa Pemba na misaada yenye thamani ya Shilingi 86,696,450 imetolewa kwa wananchi kutoka Jumuiya Muzdalifa na Al-nour.

**CHANGAMOTO ZA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR:**

*(i)* Kamati imebaini familia nyingi katika jamii hazitekelezi ipasavyo agizo la mirathi kama ilivyoelezwa katika sheria za Kiislamu, hivyo watu hurithi kwa kufuata matakwa ya kifamilia.

*(ii)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri kwa ofisi zote za Unguja na Pemba.

*(iii)* Kamati imebaini kuwepo na mwamko mdogo wa jamii katika kupeleka masuala ya mirathi katika Kamisheni hivyo kurithi kienyeji na kusababisha migogoro katika familia zao.

*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa uchakavu wa majengo na usimamizi usioridhisha wa mali za Wakfu kwa Unguja na Pemba.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

*(i)* Kamati inashauri ofisi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuetekeleza jukumu la mirathi kwa wakati na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na dini ya Kiislamau.

(ii) Kamati inashauri ofisi ya Wakfu kufuatilia kikamilifu suala la usafiri ili kujenga mazingira bora ya utekelezaji wa kazi zao.

(iii) Kamati inashauri ofisi ya Wakfu kufuatilia na kusimamia kikamilifu mali zake za Wakfu ikiwemo mashamba na nyumba wanazokodisha.

(iv) Kamati inashauri Ofisi ya Wakfu kufuatilia wapangaji wasiolipa kodi kwa wakti kwenye nyumba na maduka na kuwachukulia hatua zinazostahili.

(v) Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa moyo wa huruma watendani wa Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana katika kuboreshwa maslahi yao, kwani ofisi hii inatoa mchango mkubwa katika ukusanyaji wa mapato ya nchi.

## 2.9 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Tume ya Utumishi Serikalini ni chombo kinachojitegemea kilichoanzishwa na Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 chini ya kifungu 117 Toleo la 2010 na kifungu 33 cha Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011. Tume kwa ujumla ina jukumu la kusimamia Utumishi katika Serikali kwa uadilifu na kufuata misingi ya Utawala Bora. Tume imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuidhinisha ajira ya mkataba kwa watumishi 17, Kuthibitisha kazi watumishi 720, kupandisha daraja watumishi 197 na kubadilisha kada watumishi 50;

(b) Kuwastafisha kazi kwa lazima watumishi 232, kuwastafisha kwa hiyariwatumishi 12, watumishi wanne (4) kwa maradhi na kuridhia kuacha kazi watumishi watatu (3) kwa mujibu wa Kanuni ya 25 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014;

(c) Kupokea, kusikikiliza na kuyatolea maamuzi malamiko matatu (3) na kuidhinisha kufukuzwa kazi watumishi wawili (2) na kuachisha kazi watumishi wawili (2).

### CHANGAMOTO ZA TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

(i) Kukosekana kwa Ardhilhali za watumishi wakati wa kuwasilisha maombi ya kustaafu, kutofautiana kwa miaka ya

kuzaliwa mtumishi kati ya Ardhilhali na vielelezo vyengine kama kitambulisho cha Mzanzibar, cheti cha kuzaliwa na ZSSF.

*(ii)* Uelewa mdogo wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake.

*(iii)* Kuwepo kwa ukosefu wa mfumo wa kielektroniki wa maombi ya ajira mfumo ambao utaondosha mrundikano wa nyaraka hasa za maombi ya ajira katika Ofisi.

*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la watumishi kubadili kada ya utumishi bila kufuata taratibu za kiutumishi.

*(v)* Uchache wa vyumba na ofisi na hasa itakapoanza kutekeleza muundo mpya ambao utalazimu kuongeza idadi ya wafanyakazi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

*(i)* Kamati inashauri Tume kutoa elimu ya uelewa wa sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni zake kwa watumishi wote wa sekta za umma;

*(ii)* Kamati inashauri Tume kutoa uelewa kwa watumishi juu ya mikataba ya kazi pamoja na mambo yote muhimu yanayohusiana na utumishi kama vile ardhilhali na barua ya kuthibitishwa kazi.

*(iii)* Kamati inashauri Tume kuandaa utaratibu maalumu utakaozisaidia Taasisi kusomesha watumishi wao bila kuathiri utendaji wa Taasisi hizo kutokana na upungufu wa watendaji wakati wa masomo.

*(iv)* Kamati inashauri Tume kuweka mpango maalumu wa kuzitembelea Taasisi za Umma pamoja na kufanya ukaguzi kwa watumishi na kada zao ili kupunguza changamoto ya uhaba wa watumishi katika Taasisi za Umma.

*(v)* Kamati inashauri Tume kufuatilia moja kwa moja katikaTaasisi za Umma ili kubaini Taasisi ambazo zinachelewesha watumishi wao kuwafanyia mafunzo ya awali (induction course) na kuwachukulia hatua  za kinidhamu wakuu wa Taasisi hizo

ambao hawatekelezi agizo hilo kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.

*(vi)* Kamati pia, inashauri Tume kuyafanyia kazi mapendekezo ya upandishwaji wa madaraja ya watumishi wa umma kwa kuzingatia utaratibu na miongozo ya kiutumishi ili kupunguza malalamiko ya watendaji kwa Serikali.

## 2.10 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Kwa upande wa Kamisheni Shughuli zifuatazo zimefanyika:

*(a)* Kuridhia Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi kutoka Taasisi za Umma tatu (3). Taasisi hizo ni Shirika la Magazeti la Zanzibar, Mamlaka ya kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na Wakala wa Barabara Zanzibar;

*(b)* Kusimamia na kufuatilia masuala ya kiutumishi katika Wizara 16 na Mashirika 10 Unguja na Pemba kwa lengo kuangalia uzingatiwaji wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma katika masuala ya kiutumishi ili kuongeza ufanisi katika Utumishi wa Umma;

*(c)* Kupokea Rufaa sita (6) na kuzitolea uamuzi. Rufaa hizo zilihusu madai ya kufukuzwa kazi na madai ya maslahi mbali mbali.

## 2.11 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO

Wakala wa Serikali Mtandao ni taasisi iliopo chini ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Nambari 12 ya mwaka 2019. Lengo kuu ni kusimamia na kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Utumishi wa Umma na kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi na kijamii. Katika kutekeleza majukumu yake Wakala imetekeleza mambo yafuatayo:-

*(a)* Kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Wateja ambao kwasasa upo katika hatua za mwisho kukamilika,

*(b)* Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa Mshauri elekezi wa kuandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano ya Serikali Mtandao “e-Government Strategy”

(c) Katika kusimamia masuala ya manunuzi ya mifumo na vifaa vya TEHAMA katika Utumishi wa Umma Wakala wa Serikali Mtandao imepokea maombi (8) ya ununuzi wa vifaa ambapo maombi (5) yameidhinishwa na maombi (3) yamerejeshwa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

(d) Kupokea maombi sita (6) ya uanzishaji wa mifumo mipya na kuyafanyia kazi ambapo maombi (3) ya yamekubaliwa na maombi (3) yalirejeshwa kwa kuimarisha zaidi.

(e) Kusimamia mifumo katika taasisi za umma. Mifumo miwili (2) ambayo inasimamiwa ni Mfumo wa ZanMalipo ambapo hadi saa taasisi 4 ndio zimeanza kutumika mfumo huo, mfumo wa "Integrated Human Resource and Payroll System" upo katika hatua ya utengenezaji (development phase) na unatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi wa Disemba.

(f) Kufanya tathmini na kwa Taasisi 20 za Umma kuangalia huduma zinazotolewa ili kuweza Wakala kuja na mpango madhubuti wa uwekezaji wa mifumo ya TEHAMA.

(g) Kutengeneza mifumo mitatu ya kutolea huduma kwa njia ya kieletroniki. Mfumo wa "e-Office" unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi wa Novemba na kuanza kutumiwa na taasisi za umma, mfumo wa "Government Mail System – GMS" umeshakamilika na umeanza kutumika na mfumo wa "ICT Resources Management ictresources.egoz.go.tz" imeshakamili na unatumika hadi sasa taasisi (47) zimeshasajili rasilimali TEHAMA za taasisi zao.

**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR**:

Wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Wakala wa Serikali Mtandao ilikumbana na changamoto zifuatazo:-

(i) Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la Rasilimali Fedha: Makadario ya matumizi kwa mwaka ambayo Wakala hupangiwa ni madogo na hayatoshelezi kwa Wakala kutekeleza majukumu yake. Aidha, Wakala bado haina ruzuku (subvention) hadi sasa na matokeo yake ruzuku za Wakala zinapitia kwenye fungu la Katibu Mkuu.

(ii) Kamati imebaini kuwepokwa tatizi katika kituo cha taarifa (Data Center): Ili Wakala iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi inahitaji kuwa na sehemu ya kuhifadhia taarifa mbali

mbali za kimtandao za Serikali pamoja na "hosting" ya mifumo ya Serikali.

*(iii)* Kuwepo kwa changamoto ya Muundo wa Wakala; Pamoja na kuandaa muundo na kuuwasilisha katika mamlaka husika kwa kuidhinishwa, Wakala imechelewa sana kupata muundo wa kiuendeshaji tangu ilipoanzishwa mwaka 2019.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Ili kufikiwa lengo na dhamira ya kuanzishwa kwa Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kuipatia ruzuku kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa shughuli zake;

*(ii)* Kamati inaishauri Seriklai kuiwezesha Wakala kwa kuwa na kituo chao cha Taarifa (datacenter) hapa Zanzibar ili kwenda sambamba na mabadiliko ya ulimwengu.

*(iii)* Kamati inashauri Taasisi inayohusika na miundo kuharakisha kuidhinisha kwa muundo wa Wakala ambao utawasaidia kupata divisheni na vitengo mbali mbali ambavyo vitasaidia kufanyakazi kwa uweledi na umakini zaidi.

## 2.12 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR – ZAECA

Mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar imeundwa kwa sheria Nam. 1 ya mwaka 2012 ambapo jukumu la msingi la mamlaka hii ni Kuzuia Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar.

Katika utekelezaji wa majukumu yake Mamlaka imeweza kufanikisha mambo yafuatayo:-

*(a)* Kupokea jumla ya tuhuma 20 ambazo zinahusiana na kushawishi, kuomba na kupokea rushwa, ubadhirifu wa mali na mapato, matumizi mabaya ya Ofisi, magendo, matumizi mabaya ya mali na kukwepa kulipa kodi;

*(b)* Kutoa elimu katika Taasisi kumi na saba (17) za Serikali na taasisi zisizo za kiserikali kwa Maafisa wa kikosi cha Zimamoto, Wakufunzi na Watendaji na wanaharakati wa mapambano ya udhalilishaji wa kijinsia;

(c) Kuokoa na kurejesha kiasi cha shilingi 58,450,000 kupitia makosa mbali mbali kama vile magendo matumizi mabaya ya mali na mapato na matumizi mabaya ofisi.

**CHANGAMOTO ZA ZAECA:**

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba mkubwa wa wataalamu wa fani mbali mbali jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi zao za kupambana na uhalifu.

*(ii)* Kamati pia, imebaini kuwepo kwa changamoto ya vifaa vya kisasa vya kiuchunguzi katika maeneo kama vile bandarini na uwanja wa ndege.

*(iii)* Vile vile, mamlaka inakabiliwa na changamoto ya jengo la ofisi katika makao makuu lakini kwa upande wa ofisi za Pemba.

*(iv)* Kamati pia imebaini kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri kama vile magari kwa ajili ya ufuatiliaji na uchunguji wa uhalifu.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Ili kuepuka changamoto ya kudumu ya ukosefu wa ofisi, Kamati inashauri Mamlaka kusimamia kikamilifu upatikanaji wa eneo la ujenzi wa ofisi yao ili kuondosha changamoto ya ofisi.

*(ii)* Kamati inashauri ZAECA kuzidi kuimarisha watendaji wake kwa kuwapatia elimu na mafunzo ya kutosha ya kukabiiana na uhalifu wa uhujumu uchumi.

*(iii)* Kamati pia, inaishauri ofisi ya ZAECA kushirikiana kikamilifu na ZBS katika kudhibiti matumizi ya bidhaa zilizopitiwa na wakati.

*(iv)* Kamati inaishauri Serikali kusaidia upatikanaji wa vyomb vya usafiri kwa ZAECA ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yao.

## 2.13 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ina jukumu la kuratibu mambo yanayohusu Baraza la Mapinduzi pamoja na Kamati zake ikiwepo Kamati ya Makatibu Wakuu *(Inter Ministerial Technical Committee - IMTC).*

Ofisi hii inatekeleza majukumu yafuatayo:

*(a)* Kuandaa mikutano ya Baraza la Mapinduzi na kutunza taarifa za mikutano.
*(b)* Kuchambua nyaraka zitazowasilishwa Baraza la Mapinduzi na Kamati zake.
*(c)* Kuwasilisha maamuzi na maelekezo kwa taasisi za utumishi wa umma zinazohusika.
*(d)* Kutoa msaada wa kufanya utafiti kwa Baraza la Mapinduzi katika mambo yanayongoja au yanayotarajiwa kuwasilishwa katika Baraza hili.
*(e)* Kutekeleza majukumu mengine yoyote kama Katibu Mkuu Kiongozi atakavyoona inafaa ikiwemo kuendesha programu za kujenga uwezo kwa viongozi wa ngazi za juu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(a)* Kamati inashauri ofisi hii kusimamia na kutoa kipaumbele cha mafunzo kwa watendaji wa Serikali ili kupata wataalamu wakutosha watakaoisaidia Serikali katika kuinua uchumi wa nchi. Sambamba na hilo Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya baadhi ya Taasisi za umma kuruhusu watendaji kwenda masomoni bila kuzingatia idadi ya watendaji wanaohitajika kubakia katika kutoa huduuma.

*(b)* Aidha, katika kujenga utawala bora na utawala wa kisheria, Kamati inashauri watendaji ambao watachukua likizo na kuingia katika siasa baada ya kumaliza harakati zao za kisiasa waruhusiwe kurudi katika utendaji kwa kufuata utaratibu wa kisheria ili kuepuka malalamiko na upungufu wa wataalamu katik asekta za umma.

*(c)* Kamati inashauri kuchukuliwa hatua kwa Taasisi zote za umma ambazo zinachelewesha kutoa taarifa kwa wakati wanapotakiwa kufanya hivyo ili kujenga tabia njema kwa watendaji na wakuu wa Taasisi hizo.

## 2.14 WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kusimamia Sera, Sheria na Kanuni za Ofisi ili kuhakikisha kuwa inaweka mazingira mazuri ya kutoa huduma za kijamii na kiuchumi na vile vile kuimarisha ulinzi na usalama kwa wananchi na wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar. Aidha, Ofisi hii ina jukumu la kuratibu na kusimaia shughuli zinazotekelezwa na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zinasaidia kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa wananchi.

*Dira* ya Ofisi hii ni kuwa Taasisi imara katika kusimamia amani, usalama, usajili wa wakaazi na upatikanaji wa huduma karibu na wananchi.

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na Idara zifuatazo zilizo chini Katibu Mkuu:

*(a)* Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa.
*(b)* Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ.
*(c)* Tume ya Utumushi wa Idara Maalum za SMZ.
*(d)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(e)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
*(f)* Ofisi Kuu Pemba.

Aidha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inasimamia Taasisi *11* zinazojitegemea zifuatavyo:

*(i)* Jeshi la Kujenga Uchumi *(JKU),*
*(ii)* Chuo cha Mafunzo *(MF),*
*(iii)* Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo *(KMKM),*
*(iv)* Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU),
*(v)* Kikosi cha Valantia *(KVZ),*
*(vi)* Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi,
*(vii)* Ofisi ya Mkoa wa Kusini Unguja,
*(viii)* Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja,
*(ix)* Ofisi ya Mkoa wa Kusini Pemba,
*(x)* Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba,
*(xi)* Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

## 2.15 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

## 2.16 JESHI LA KUJENGA UCHUMI *(JKU)*

Jeshi la Kujenga Uchumi *(JKU)* limeanzishwa chini ya kifungu cha *121(1)* cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* pamoja na Sheria nambari *6* ya mwaka *2003*.

Kwa mujibu wa Sheria, JKU imepewa jukumu la kutoa mafunzo kwa vijana katika nyanja za uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, kuwafunza vijana ufundi, kazi za amali na uzalendo kwa ajili ya kuwafanya vijana hao waweze kujitegemea, kuitumikia na kuijenga nchi.

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa kufanikiwa kutoa mafunzo ya uzalendo na ukakamavu kwa Vijana 2,778 katika Kambi za JKU Unguja na Pemba.

Aidha, JKU limetoa mafunzo ya kazi za amali kwa vijana 1,268 ambapo mafunzo hayo yametolewa kupitia Skuli ya Ufundi JKU Mtoni na Wanafunzi 1,249 wameendelea na masomo ya michipuo ya Sanaa, Sayansi, Sayansi ya Kompyuta, Ufundi na Biashara katika Skuli ya Sekondari JKU Mtoni.

Vile vile, Kamati imeridhishwa na hali ya ujenzi wa mahanga ya askari kwa upande wa Pemba pamoja na kuwepo kwa mazingira bora yenye mashirikiano ya utendaji kazi kwa askari na wakuu wa Jeshi katika kambi zote za Unguja na Pemba.

## 2.17 WAKALA WA ULINZI WA JKU:

Wakala wa Ulinzi wa JKU umeanzishwa kwa lengo la kutoa ulinzi kwa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Wakala umekuwa na mchango mkubwa katika mapato ya Serikali lakini pia, umeweza kuimarisha ulinzi na kupunguza matukio mengi ya kihalifu katika maeneo mbali mbali ikiwemo mahotelini na makampuni binafsi.

**CHANGAMOTO ZA JESHI LA KUJENGA UCHUMI:**

*(i)* Kuwepo kwa muwekezaji wa kilimo kutoka nchini misri ambae amekuwa akitumia shamba la JKU kwa shughuli zake za uwekezaji katika sekta ya kilimo pamoja na kutumia rasilimali watu wa JKU kwa shughuli zake binafsi kama vile madereva, wapishi na walinzi bila ya kulipia fidia yoyote kwa JKU au Wizara husika.

*(ii)* Uhaba wa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri, pamoja na zana za kilimo, matrekta, pawatila, majembe ya kuchimbulia kuburugia na kupanda.

*(iii)*Kukosekana kwa maji ya uhakika ya visima na badala yake kutegemea mvua ambazo huathiri sana shhughuli za kilimo.

*(iv)*Urasimu wa michakato ya zabuni za serikali ambao huchelewesha uanzaji kazi za maendeleo.

*(v)* Ukosefu wa gari la kubebea wagonjwa pamoja na uhaba wa dawa na vifaa mbalimbali vya uchunguzi wa magonjwa na mashine ya usingizi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA JKU**

*(i)* Kamati inashauri JKU kufanya utafiti wa kina kwa kambi zote za Unguja na Pemba na kufahamu ni uzalishaji wa aina gani unahitajika kwa kila kambi badala ya kufanya kazi za uzalishaji bila kufanya utafiti, kwani Kamati imebaini zipo baadhi ya Kambi zinajihusisha na kilimo cha mboga mboga na matunda bila kuangalia mazingira halisi ya maeneo hayo. Mfano wa Kamabi hizo ni JKU Makangale, JKU Pujini na JKU Chokocho. Kambi hizi ni vyema kujishughulisha na ufugaji pekee kuliko kilimo cha mazao na mboga mboga.

*(ii)* Aidha, JKU ni vyema kuandaa wataalamu wa kutosha kuhusiana na fani za Kilimo na Ufugaji ili kuzalisha kwa kiwango kikubwa na kuacha kulima na kufuga kimazoea ambako hawapati tija yoyote kama jeshi. Kamati imebaini zipo baadhi ya Kambi zinafuga bila kuzingatia utaalamu wala kutoa kipaumbele cha ufugaji na hivyo, kupelekea uzalishaji mdogo usio na manufaa.

*(iii)* Kamati imesikitishwa na hali ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa baadhi ya Kamabi za JKU na hivyo kuhatarisha maisha ya askari wetu. Katika ziara ya Kamati ya kambi ya Chokocho Mkoa wa kusini Pemba Kamati haikuridhishwa na hali ya maji yanayotumiwa katika kambi hiyo, hivyo tunashauri JKU Makao Makuu kwa kushirikiana na Wizara kulisimamia suala hili kwa haraka na kuhakikisha kambi hii imepata maji safi na salama kama ilivyo kwa kambi nyengine.

*(iv)* Kwa upande wa JKU Cheju eneo ambalo linategemewa kutumika zaidi kwa uzalishaji wa mpunga na mboga mboga; Kamati inashauri Serikali kusaidia juhudi zao za upatikanaji wa maji ya uhakika pamoja na upatikanaji wa nishati ya umeme kama hatua itakayosaidia katika kilimo cha umwagiliaji.

*(v)* Kamati inashauri Serikali kujengea uwezo Wakala wa Ulinzi wa JKU ili iweze kumudu shughuli zote za ulinzi nchini kwa vile kutokana na maendeleo yaliopo ulimwenguni, kunahitajika ulinzi wa kitaalamu unaotumia zana za kisasa.

*(vi)* Kamati inashauri Serikali kuzitaka taasisi zote za Serikali kulindwa na Wakala wa Ulinzi wa JKU na kuepusha ulinzi unaofanywa kwa kutumia mazoea.

*(vii)* Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ inashauriwa kushughulikia suala la madeni yanayodaiwa na Wakala katika taasisi mbali mbali ili Wakala uweze kuendesha shughuli zake kama inavyojipangia.

*(viii)* Kamati pia, inashauri Serikali kuangalia vyema uwepo wa kampuni binafsi za ulinzi nchini na kutoa muongozo sahihi juu ya uendeshaji wa kampuni hizo.

*(ix)* Mwisho, Kamati inashauri Serikali baada ya kukamilisha zoezi la ujenzi wa nyumba za askari sasa iangalie kwa umuhimu wake upatinaji wa usafiri wa uhakika kwa JKU Unguja na Pemba ili kuondosha changamoto hii ya muda mrefu.

## 2.18 CHUO CHA MAFUNZO (MF)

Chuo cha Mafunzo *(MF)* ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari *1* ya mwaka *1980* na Sheria nambari *3* ya marekebisho ya mwaka *2007*. Idara hii ina jukumu kubwa la kuwapokea wale wote wanaoletwa Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa Sheria, kuwalinda pamoja na kuwarekebisha tabia ili wanaporudi katika jamii wawe raia wema.

Katika kutekeleza programu ya urekebishaji tabia kwa kipindi cha July –Septemba Chuo (Gereza) kimepokea jumla ya wanafunzi na mahabusu 663 (kwa 2021/22) kati yao wanafunzi 165 na Mahabusu 498 ambapo hadi kufikia 31 septemba jumla kuu ya wanafunzi na Mahabusu ilikua ni 943.

Hata hivyo, kufikia Septemba 2021/22 kambi ya Kiinua Miguu imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

*(a)* Kuendelea kuwapatia elimu ya mafunzo ya amali wanafunzi walioko chuoni mfano ufundi kuchonga, ufundi kujenga, ufundi gereji, ufundi wa kushona nguo, kilimo pamoja na ufugaji.

*(b)* Kuendelea na kisomo cha watu wazima (PEP) kwa wanafunzi na Mahabusu wasiojua kusoma,kuandika pamoja na kuhesabu (3k) ambapo kwa sasa kuna jumla ya wanafunzi wapatao 43. Katika kuboresha vyanzo vya mapato, Chuo kimejenga banda jipya kwa ajili ya ufugaji wa mabata sambamba na ujenzi wa banda jipya kwa ajili ya Gereji.

**CHANGAMOTO ZA CHUO CHA MAFUNZO:**

Licha ya mafanikio mazuri yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Chuo cha Mafunzo Zanzibar kimekabiliwa na Changamoto zifuatazo:-

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa upungufu wa magodoro na mablangeti ya kulalia wanafunzi na rimande kwa magereza yote ya Unguja na Pemba.

*(ii)* Kuwepo kwa uchakavu wa gereza la Kiinua Miguu ambalo limejengwa tangu enzi za wakoloni linapelekea kuvuja na kuhitaji fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati.

(iii) Kamati imebaini kuwepo kwa mrundikano mkubwa wa rumande chuoni unaotokana na ucheleweshwaji wa mwenendo wa kesi mahakamani (proceed) pamoja na ongezeko la kesi za udhalilishaji.

(iv) Kuwepo kwa ongezeko la Wanafunzi wengi katika chuo cha urekebishaji tabia cha Kiinua Miguu wasioweza kufanya kazi mfano wagonjwa wa HIV, TB na watumiaji wa dawa za kulevya (mateja).

(v) Aidha, Kamati imebaini kuweopo kwa uchakavu wa vitendea kazi, mfano magari mengi ni mabovu na hayakidhi mahitaji ya Chuo cha Mafunzo.

(vi) Upungufu wa vifaa tiba hasa vya uchunguzi wa afya za binaadamu ni tatizo kwa upande wa huduma za afya.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Katika kukabiliana na changamoto hizo Kamati inashauri yafuatayo:

(i) Kufanyiwa ukarabati mkubwa wa Chuo cha urekebishaji tabia Kiinua Miguu ikiwemo kuboresha miundo mbinu ya ndani na nje ya chuo.

(ii) Kamati inashauri Taasisi inayohusika na uendeshaji wa Kesi za jinai kuhakikisha zimendeshwa kwa haraka ili kupunguza idadi kubwa ya mahabusu.

(iii) Kamati inashauri Serikali ione uwezekano wa kutumia adhabu mbadala ikiwemo vifungo vya nje ni utaratibu wa kisheria na kawaida hiyvo, kuwepo usimamizi maalum wa kutoa adhabu mbadala na kuzisimamia ili kupunguza mrudikano wa wanafunzi vyuoni.

(iv) Kamati inashauri Serikali kuwapatiwa gari mpya Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya kuwapelekea na kuwarudisha wanafunzi pamoja na mahabusu Mahakamani

(v) Serikali kupitia wizara ya Afya kusaidia upatikanaji wa vifaa tiba kama vile microskop na vifaa vyengine ili kudhibiti ongezeko la maradhi katika magereza yetu.

(vi) Kuwepo kwa desturi ya matumizi ya mitondoo ndani ya chuo cha urekebishaji tabia Kiinua Miguu na magereza mengine ni kukiuka haki za binaadam, hivyo Kmati inashauri Serikali

iliangalie suala hili kwa jicho la huruma kwa kuboresha miundo mbinu ya vyoo na majitaka.

## 2.19 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo *(KMKM)* kimeanzishwa chini ya Sheria nambari *1* ya mwaka *2003* ambapo kina majukumu ya kulinda usalama wa bahari ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, kuzuia njia zote zinazoweza kutumika kupitishia magendo, kusaidia vyombo vya baharini vya abiria na kufanya uokozi baharini pamoja na kushirikiana na Jeshi la Wananchi pale itakapotakiwa kufanya hivyo katika kuilinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kikosi cha KMKM kimefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:

*(a)* Kuimarisha shughuli za Ulinzi wa Bahari na nchikavu kwa kufanya doria mbali mbali na kufanikiwa kukamata baadhi ya mali za magendo katika juhudi za kupambana na uhujumu wa uchumi.

*(b)* Kuimarisha malazi bora kwa Maafisa na Wapiganaji. Katika hatua hii Kamati inapongeza sana juhudi za KMKM kwa kuimarisha makaazi ya Askari wake pamoja na ofisi kwa upande wa Pemba.

*(c)* Kutoa chakula bora kwa Maafisa na Maaskari waliopo kambini kwa Kamandi zote za Unguja na Pemba.

*(d)* Kutoa huduma za afya bora kwa Maaskari na raia wa mijini na vijijini pamoja na kuimarisha huduma kwa Hospitali kuu ya KMKM Mtoni.

### CHANGAMOTO ZA KIKOSI CHA KMKM:

Licha ya mafanikio kadhaa ambayo Kamati imeyaona na kukubaliana na juhudi ambazo wanazichukua katika utekelezaji wa majukumu yao, hata hivyo KMKM imekabiliwa na changamoto zifutazo:-

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa madawa na vifaa tiba kwa vituo vya mashamba jambo linalopelekea usumbufu kwa askari wanaoishi kambini. Uhaba huu umejitokeza zaidi Kambi

ya Unguja Ukuu kutokana na kuwepo askari wengi kambini pamoja na jamii inayowazunguka kutumia kituo hiki kwa huduma za mama na mototo. Kambi ya Chokocho, Kambi ya Likoni, Kambi ya Msaani kwa upande wa Pemba.

*(ii)* Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa ubovu wa miundo mbinu ya Umeme katika Kambi mbali mbali za Unguja na Pemba.

*(iii)* Ubovu wa barabara za kuingilia Kambini imekua changamoto kubwa katika utekelezaji wa majukumu yao. Kamati imebaini changamoto hii katika Kamabi ya Kama, kambi ya Chokocho na Kambi ya Maziwa Ngo'ombe.

*(iv)* Vile vile, Kamati imebaini kuwepo na uhaba wa Ofisi za wakuu wa Kikosi kwa baadhi ya Kambi za Unguja na Pemba kama vile Kambi ya Unguja Ukuu, Tundauwa.

*(v)* Pia, Kamati imeelezwa kuwepo kwa tatizo la boti za uhakika za operesheni wa Magendo, mashine kwa ajili ya doria za ulinzi na uokozi baharini.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuipatia mgao wa dawa na vifaa tiba kutoka Serikalini Hospitali ya KMKM Kibweni kutokana na kuwa Hospitali hiyo imepandishwa hadhi kutoka kuwa Kituo cha Afya na kuwa Hospitali kwa sasa na kuongezeka kwa watu wanaotaka huduma Hospitalini hapo.

2. Kikosi cha *KMKM* kinashauriwa kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu yake kutoka na kukuwa kwa shughuli zake hapo Kibweni na kupelekea ufinyu wa ofisi kwa viongozi na wapiganaji wake.

3. Kamati inashauri kikosi kusimamia kikamilifu upatikanaji wa vifaa tiba kwa kambi za mashamba Unguja na Pemba ili kuimarisha huduma za afya na kuwajengea mazingira bora askari waliopo vituoni.

4. Kamati inashauri Serikali kulitatua tatizo la miundo mbinu ya umeme kwa kuwatumia wataalamu wa shirika la umeme kushauri

na kuimarisha huduma za umeme katika kambi zote zenye mapungufu kama haya.

5. Katika kukabiliana na changamoto ya ubovu wa barabara za kuingilia kambini kama vile Kambi ya Kama, Chokocho, Maziwa Ng'ombe na Msuka, Kamati inashauri barabara hizi pia kuingizwa katika mpango wa matengenezo wa barabara za ndani kwani hutumika pia na wananchi wa maeneo haya.
6. Kamati pia, inashauri suala la doria kupewa kipaumbele kwa kuimarisha huduma za usafiri na kujenga mashirikiano na wananchi wa ukanda wa pwani kwani taarifa nyingi zitapatikana kupitia kwao.

## 2.20KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi *(KZU)* kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari ***7*** ya mwaka *1999* na kina jukumu la kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za watu, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto kwenye Viwanja vya Ndege na Bandarini zinakwenda sambamba kulingana na masharti ya Kitaifa na Kimataifa.

***Utekelezaji wa shughuli za Maendeleo (Miradi).***

Kwa upande wa miradi katika kipindi cha julai-Septemba Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiliendelea na utekelezaji wa mradi wake mmoja wa ujenzi kwa kituo cha Zimamoto na Uokozi Kijichame pamoja na Mahanga ya Wapiganaji wa Zimamoto na Uokozi. Kamati imeelezwa kuwa uendelezaji wa mradi huo umefikia asilimia tisiini (90%) na ulisimama kwa muda kutokana na changamoto kadhaa zilizojitokeza.

***Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kikosi cha Zimamoto Zanzibar:***

Katika kipindi kipindi cha july – septemba, 2021 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

*(a)* Kikosi kimefanikiwa kuanza kutoa huduma katika Wilaya ya Micheweni baada ya kupata gari mpya ya kutolea huduma ya uzimaji moto na kufikia azma ya serekali kusogeza huduma karibu na wananchi.

(b) Kikosi kimefanikiwa kutoa huduma katika matukio yote ya ajali za moto na ajali nyengine na kuokoa maisha ya watu na mali zao kwa kushirikia na raia wema waliokuwa karibu ya matukio.

(c) Kikosi kimefanikiwa kupata maeneo mawili (Finya na Wete) kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa Kasikazini Pemba na Mkoa wa Kusini Pemba kwa ajili ya ujenzi wa vituo na mahanga ya wapiganaji.

(d) Kikosi kimefanikiwa kutoa elimu kwa taasisi za kiserikali na binafsi juu ya majanga ya moto na jinsi ya kujikinga.

(e) Kikosi kimefanya ukaguzi katika taasisi mbalimbali za Serikali na Taasisi binafsi na kuona jinsi zilivyojipanga kukabiliana na hali za dharura za majanga ya moto.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI PEMBA.**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi kifupi cha miezi mitatu bado kuna changamoto kadhaa zinazowakabili KZU kwasasa, miongoni mwa hizo ni hizi zifuatazo:-

(i) Kamati imebaini kuwepo kwa uchakavu mkubwa wa magari ya kuzimia moto katiuka vituo mbali mbali, pia yapo baadhi ya magari hayafanyi kazi kutokana na mapungufu ya kitaalamu.

(ii) Pia, Kamati imebaini lipo tatizo la uchelewaji wa kutoa taarifa kwa wananchi linapotokea janga la moto katika makaazi ya watu.

(iii) Kama ilivyo kwa vikosi vyengine vya Zanzibar katika kikosi hiki pia kimekabiliwa na ubovu wa miundo mbinu ya barabara hususan barabara za ndani na hivyo kufanya ugumu wa kutoa huduma wakati wa dharura.

(iv) Na mwisho, Kamati imebaini kuwepo kwa uchache wa vituo vya kuzimia moto hali inayopelekea ugumu wa kufika eneo la tukio na kuchelewa kwa waokozi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inashauri Serikali kuandaa mpango maalumu utakaowezesha KZU kupata magari ya kutosha ya kuzimia moto pamoja na vifaa vya kisasa vitakavyosaidia kupambana na majanga ya moto.

2. Kamati inashauri KZU kuzidi kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutoa taarifa kwa wakati mara tu linatokea tatizo la maafa. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kuweka mikakati maalumu ya kuwashughulikia watu wanaotoa taarifa za uongo za moto na maafa katika jamii.

3. KZU wapatiwe mafunzo ya kitaalamu ya kupambana na majanga haya ili kuepusha kutumia njia za kienyeji ili kunusuru maisha ya watu.

## 3.7 KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ)

Kikosi cha Valantia *(KVZ)* kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari *5* ya mwaka *2004* na kina majukumu ya kuweka amani na utulivu nchini, kupambana na janga lolote litakaloikumba jamii, kulinda viongozi na mali za Serikali na kufanya kazi za kijeshi kwa madhumuni ya kuzuia hali inayohatarisha ulinzi na usalama.

***Utekelezaji wa shughuli za Maendeleo kwa KVZ***

Kikosi cha Valantia zoni ya Pemba kilipanga kutekeleza kazi za ujenzi wa hanga la askari katika kambi ya Pujini ujenzi ambao hadi sasa unaendelea katika hali nzuri.

*(i)* Kikosi cha Valantia kilipanga kujenga kituo kimoja cha zahanati kwa upande wa Pemba lakini bado lengo hili halikufikiwa kutokana na changamoto ya kifehda.

*(ii)* Pia, Kamati imeelezwa kuwepo kwa mpango wa ujenzi wa nyumba ya mkuu wa Kambi ya Pujini ambapo hadi kufikia mwezi wa Disemba 2021 kazi hii haikuweza kufanyika.

**CHANGAMOTO ZA KIKOSI CHA VALANTIA:**

**Kikosi cha Valantia Zoni ya Pemba** kinakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo: -

*(i)* Ubovu wa Barabara ya kuingilia Kambini Ndugukitu.
*(ii)* Ukosefu wa nyumba za kulala Maafisa.
*(iii)* Ukosefu wa Zahanati kwa ajili ya Wagonjwa.
*(iv)* Ukosefu wa Mahanga ya kulala Askari Micheweni.
*(v)* Ukosefu wa usafiri kwa kambi za KVZ hususan zoni ya Pemba.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Kamati inashauri Serikali kuunga mkono jitihada za kikosi kwa kuwapatia fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa wakati na kwa mujibu wa matumzi yao ya kila mwezi ili wapate kutekeleza kazi zao kama walivyojipangia.

*(ii)* Kamati inashauri Kikosi kufanya juhudi za makusudi katika kupambana na changamoto ya ukosefu wa zahanati.

## 3.8 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mkoa wa Mjini Magharibi ni miongoni mwa Mikoa mitano ya Zanzibar ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 2(a) na Sheria Nambari 08/2018 Sheria ya Tawala za Mikoa. Kiutawala Mkoa wa Mjini Magharibi ni mkusanyiko wa Wilaya tatu; (Mjini, Magharibi 'A' na Magharibi 'B') na Shehia 121 ukiwa na jukumu la kusimamia na kutekeleza Sera, Sheria, Mipango na Miongozo ya Serikali.

**MAFANIKIO YA UTEKELZAJI WA MAJUKUMU YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI**

Katika kipindi cha Juali – Disemba, 2021 Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja umefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo kwa mujibu wa sharia na taratibu za Tawala za Mikoa Zanzibar, miongoni mwa majukumu hayo ni haya yafuatayo:-

*(a)* Kuimarisha masuala ya Ulinzi na Usalama, jumla ya vikao 38 (24 vya kawaida na 14 vya dharura) vilivyojadili hali ya usalama

kiujumla na kupanga mikakati ya kuondoa changamoto za kiusalama zilizojitokeza katika kipindi hicho zikiwemo vitendo vya unyang'anyi, wizi wa mazao na vitendo vya udhalilishaji ndani ya Mkoa. Katika kutekeleza mikakati hiyo doria za usiku zilifanyika katika Shehia 17 ikiwemo Kisiwandui, Kikwajuni juu, Mboriborini, Amani, Kwahani, Muembe Tanga, Fumba, Nyamanzi, Kinuni na Jumbi kwa lengo la kupunguza vitendo vya uhalifu wa ukabaji na shughuli za starehe zinazofanywa kinyume na utaratibu uliowekwa ambapo jumla ya watu 72 (wakiwemo Madada powa 16 na Kaka powa 8) walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

*(b)* Aidha, Mkoa uliratibu na kudhibiti wizi wa mazao na mifugo, rasilimali ya mchanga, kupunguza wimbi la migogoro ya ardhi, kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kupunguza vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto pamoja na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana kwa kuwaelimisha kutochagua kazi za kufanya katika maisha yao ya kila siku.

*(c)* Mkoa umeratibu maagizo na ahadi mbalimbali za viongozi wa SMZ na SMT zilizotolewa wakati wa ziara zilizofanywa ndani ya Mkoa. Aidha, mambo yaliyofanyika ni kufanya mikutano na taasisi za Sekta husika, ziara za kukagua utekelezaji wa maagizo hayo ambapo baadhi ya maagizo yametekelezwa na mengine yanaendelea na hatua za utekelezaji.

*(d)* Katika kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Mkoa umefanya vikao na wadau mbalimbali kujadili utekelezaji wa miradi iliyopo ndani ya Mkoa ambapo jumla ya miradi 12 inatekelezwa ndani ya Mkoa. Aidha ziara nne za kufuatilia miradi ya maendeleo zimefanywa ambapo jumla ya miradi saba (7) ilikaguliwa na kuona utekelezaji wake miradi iliyokaguliwa ni pamoja na mradi wa maji wa exim bank ya India, ujenzi wa madarasa sita (6) ya Skuli ya Mtoni Kidatu, Ujenzi wa Barabara ya Sharifmsa-Mwanyanya, mradi wa elimu TV Kwarara, Ujenzi wa Terminal 3, Ujenzi wa Soko la Malindi, Ujenzi wa madarasa sita Skuli ya Msingi Sebleni.

*(e)* Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2021 Mkoa umefuatilia matukio 313 ya udhalilishaji wa watoto yaliyoripotiwa katika ngazi za Shehia na Wilaya ambapo kesi 146 kubaka, kesi 51 kuingilia kinyume na maumbile, kesi 69 kulawiti, kesi 24 shambulio la kuumiza mwili, kesi 6 kukashifu, kesi 17

kutorosha na kesi 173 ya kutelekeza watoto. Katika matukio hayo, 32 yamepatiwa ufumbuzi, 4 yapo Mahakamani, 1 lipo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na 276 yanaendelea na hatua mbalimbali za upelelezi. Aidha, katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, Mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ulifanya mikutano 9 ya kuelimisha athari za udhalilishaji kwa skuli za msingi, madrasa na Shehia.

*(f)* Mkoa kwa kushirikiana na sekta ya Kukabiliana na Maafa umefuatilia matukio 32 yaliyoripotiwa yakiwemo (21 ya ajali za moto, manne ya upepo, moja kuzama kwa mtoto katika shimo la karo, mawili kuokotwa kwa maiti na moja kubomoka kwa ukuta uligongwa na gari) ambapo athari zilizojitokeza ni uharibifu wa makaazi, upotevu wa mali na vifo vitatu (3), wananchi waliopatwa na maafa hayo walifarijiwa kwa kupatiwa msaada wa chakula na matibabu. Pia, Mikutano miwili ya utoaji wa elimu juu ya kujikinga na maafa imefanywa.

## 3.9 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR

Baraza la Jiji la Zanzibar lilianzishwa mnamo mwaka 2019 chini ya kifungu cha 18 cha Sheria Nambari 7 ya Mwaka 2014. Majukumu ya kimsingi ya Baraza la Jiji ni yanavyoainishwa katika kifungu Nam. 19 (a-h) ya Sheria hiyo.

**UTEKELEZAJI HALISI WA MAJUKUMU YA BARAZA LA JIJI ZANZIBAR.**

Katika kipindi hiki kifupi cha mwaka wa fedha 2021/22 Baraza la Jiji limefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

*(a)* Kuandaa Mpango Mkakati wa Jiji ambao utaweka mwelekeo wa maendeleo ya Baraza kwa miaka mitano ijayo.

*(b)* Baraza limeendelea kulipa posho na stahiki nyengine za waheshimiwa Madiwani na watendaji wake kwa lengo kuimarisha mazingira bora ya kazi.

*(c)* Kwa uoande wa usimamizi wa Manispaa, Baraza la Jiji lilifanya vikao vya pamoja vinavyohimiza kufanikisha zoezi la usafi katika miji yetu.

*(d)* Baraza pia limetoa mafunzo kwa waheshimiwa Madiwani wa Baraza la Jiji pamoja na Halmashauri nyengine za Unguja na Pemba kwa lengo la kujenga uelewa wa majukumu yao. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa njia ya Mtandao na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar.

*(e)* Baraza limeshiriki katika kuwezesha uwekezaji wa ndani ya Jiji kupitia Mradi wa soko na stendi ya gari Chuini katika hatua ya ujazaji mkataba.

*(f)* Pia, Baraza liandaa pendekezo la Mradi wa Ujenzi wa Amani CCM Shopping Complex ambapo mradi upo katika hatua ya mazungumzo na mwekezaji.

**CHANGAMOTO ZINAZOLIKABILI BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR.**

Katika utekelezaji wa Bajeti, Baraza la Jiji limekuwa likikabiliana na changamoto kadhaa ikiwemo zifuatazo:-

*(a)* Kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu ambapo fedha za Matumizi Mengineyo (OC) huingizwa katika Taasisi za Serikali kwa mujibu wa umuhimu wa vipambele vya Taasisi husika.

*(b)* Ujosefu wa jengo la kudumu la Baraza pamoja na vifaa vya kufanyia kazi na vyombo vya usafiri.

*(c)* Kuwepo kwa muingiliano na mgongano wa kimajukumu na Taasisi nyengine za Umma.

*(d)* Ukosefu wa vyanzo vya mapato katika maeneo ya Jiji.

*(e)* Uhaba wa wataalamu katika sekta ya Uchumi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Licha ya changamoto mbali mbali ambazo kimsingi zinarudisha nyuma maendeleo ya Jiji la Zanzibar Kamati imeona zipo hatua ambazo zikitekelezwa zitaweza kusaidia kutatua changamoto hizo, miongoni mwa hatu hizo ni kama ifuatavyo:-

*(i)* Serikali kuchukua hatua za makusudi kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa Nambari 7 ya Mwaka 2014 ambayo itaweka muundo utakao liwezesha Baraza la Jiji kujitegemea katika eneo lake la kiutawala pamoja na kuwa na vyanzo vyake vya mapato bila kuwepo mgongano na Taasisi nyengine.

*(ii)* Kuendelea kubuni na kuibua vyanzo vya mapato na miradi ya kiuchumi na kijamii ambayo ambayo italiwezesha Baraza la Jiji kujikimu kwa kipato na hivyo kupata nguvu kiuchumi.

*(iii)* Baraza lijikite katika kusimamia majukumu ya msingi ya Baraza pamoja na kuiamarisha shughuli za utalii na uekezaji kwa kuazisha miradi ya Jiji.

*(iv)* Baraza liandae mpango maalumu utakawawezesha kupata ofisi yake ya kudumu pamoja na kuwa na wataalamu ambao watasaidia kukuza maendeleo ya Jiji.

*(v)* Baraza lizidishe mashirikiano yake na Taasisi nyengine za Serikali na zile za binafsi kwa lengo la kukuza mahusiano na kuboresha maendeleo ya Jiji.

## 3.10 BARAZA LA MANISPAA MJINI

Baraza la Manispaa Mjini limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji.

**UTEKELEZAJI HALISI WA MAJUKUMU YA BARAZA LA MANISPAA MJINI**

*(i)* Katika kuimarisha usafi wa mji Baraza la Manispaa Mjini limebinafsisha huduma za usafi kwa kampuni ya V- Clean ambapo kampuni hiyo imeanza kufanya kazi tarehe 01/07/2021 katika maeneo ya Mji Mkongwe na Magharibi. Aidha, Baraza la Manispaa Mjini kwa kushirikiana na vikundi vya Jamii na Shehia linaendelea na zoezi la kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya masoko, sehemu za biashara, maeneo ya wazi, zoni ya Kusini na Kaskazini.

*(ii)* Baraza kwa kushirikiana na kampuni ya V – Clean imezindua mifuko maalum kwaajili ya kuhifadhia taka ngumu ambayo mifuko hiyo itatumika katika maeneo ya Mji Mkongwe, maeneo ya kibiashara na maeneo ya utalii kwa majaaribio pamoja na uzinduzi wa gari saba za kuzolea taka ambazo gari hizo tayari zimeshaanza kufanya kazi.

*(iii)* Baraza, limeendelea kutoa elimu ya usafi kupitia vyombo vya habari ambapo jumla ya vipindi vitano vimerushwa hewani pamoja na matangazo nane yametolewa kupitia vyombo vya habari TV/ redio na gari ya barabani (road show). Aidha, mikutano 26 ya uhamishaji jamii juu usafi katika Shehia na wafanya biashara imefanyika sambamba na kutoa ndoo za kuhifadhia taka (Dustbin) 525 katika maeneo ya barabara, bustani, masokoni na wafanyabiashara.

*(iv)* Katika jitihada ya kuufanya mji upendeze Baraza la Manispaa Mjini linaendelea kazi ya ujenzi wa njia ya waendao kwa miguu "walk way" na kituo kidogo cha dala dala "bus stop" katika eneo la Rahaleo kuanzia skuli ya Mwembeshauri hadi skuli ya Mwembeladu.

*(v)* Katika kuimarisha mazingira bora ya wafanyabiashara wadogo, Baraza limekamilisha ujenzi wa mabanda matano ambayo yanategemewa kuchukuwa wafanyabiashara 299 pamoja na kukamilisha ujenzi wa maduka 10 katika soko la Kibandamaiti.

*(vi)* Baraza la Manispaa Mjini katika kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo limeingia katika makubaliano na kampuni ya Simba Developer Company mnamo tarehe 7/12/2021 kwa ajili ya ujenzi wa Darajani Bazaar ambao utajumuisha ujenzi wa maduka katika eneo la Donge ambapo Baraza la Manispaa Mjini linatarajiwa kupokea asilimia 25 ya makusanyo na asilimia 75 ni ya muwekezaji, mradi huo utaendeshwa kwa njia ya ubia baina ya Baraza la Manispaa na kampuni ya Simba Developer Company kwa muda wa miaka 25.

**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MANISPAA MJINI**

Licha ya mafanikio mbali mbali yaliyofikiwa katika kipindi hiki, Baraza la Manispaa Mjini linakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwemo hizi zifuatazo:-

*(i)* Kushuka kwa mapato ya Baraza kutokana na kuondolewa kwa baadhi ya vyanzo vyake vya mapato.

*(ii)* Kamati imebaini kuwepo kwa idadi ndogo ya wajasiriamali waliosajiliwa ukilinganisha na idadi kubwa ya wajasiriamali waliopo katika Baraza ambapo ni jumla ya wajasiriamali 1500 tu wamesajiliwa kati ya zaidi ya 4000 waliopo.

*(iii)* Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa upotevu mkubwa wa mapato yataokanayo na chanzo cha minara ya simu kutokana na kusitishwa kwa ufuatiliaji wa vyanzo hivyo tokea mwezi wa March, 2021.

*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa sintofahgamu miongoni mwa uongozi wa Manispaa na waheshimiwa Madiwani kutokana na kutoshirikishwa kikamilifu kwa Waheshimiwa Madiwani katika uanzishaji wa Miradi ya Maendeleo na Maamuzi yanayofanywa katika utekelezaji wa miradi hiyo.

*(v)* Aidha, Kamati imebaini kuwa elimu ndogo ya wajasiriamali na wafanyabiashara katika kulipa kodi ni miongoni mwa changamoto zinazopelekea kushuka kwa mapato ya Baraza la Manispaa Mjini.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Kutokana na changamoto mbali mbali ambazo Kamati imeziibua ambazo kimsingi zinarudisha nyuma maendeleo ya Manispaa Mjini, Kamati inashauri na kupendekeza mambo yafuatayo:-

*(i)* Baraza kuzidi kuibua vyanzo vipya vya mapato katika maeneo yake ya mjini pamoja na kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kwa kuziba mianya yote inayopelekea kushuka kwa mapato.

*(ii)* Baraza lihakikishe limeendeleza zoezi la usajili wa wajasiriamali pamoja nakuwapatia vitambulisho vya kazi kwa mujibu wa maeneo yao ili kupunguza vijana wanaozurura mitaani.

*(iii)* Serikali kupitia Wizara hii ya OR – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa izisadie Manispaa kwa kuwapatia wataalamu ambao watafuatilia ukusanyaji wa mapato

kupitia minara ya simu kwani wanaohitajika ni wataalau wabobezi katika fani za ICT na Baraza limeshindwa kuwataumia kwasababu ya ukosefu uliopo.

*(iv)* Kamati inashauri Baraza mlizidishe kasi ya usafi wa mji pamoja na ukusanyaji wa taka katika maeneo mbali mbali ya mji.

*(v)* Kamati inashauri Baraza kuwashirikisha kikamilifu waheshimiwa Madiwani katika uanzishaji wa miradi ya Maendeleo, pamoja na kulinda maslahi yao kwa kuwapatia stahiki zao kikamilifu na kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

## 3.11 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A"

Baraza la Manispaa Magharibi 'A' limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji.

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI HALISI WA BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI 'A'**

*(a)* Katika kuimarisha usafi wa Mazingira, Baraza la Manispaa Magharibi "A" limefanya ukaguzi wa baadhi ya nyumba katika Shehia 31 ambapo nyumba 385 zimekutwa zinatiririsha maji machafu ovyo na hazikua na karo ambapo wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo na wengine kutozwa faini.

*(b)* Aidha, Baraza limefanya zoezi la ukaguzi kwa wafanyabiashara 1,017 lilifanyika katika shehia zote 31 (vioski 201, mikahawa 93, mabucha 84, bekari 35, maduka ya chakula 350 na mama/baba lishe 254) ambapo wafanya biashara 99 walikutwa na makosa na kuchukuliwa hatua kulingana na makosa yao.

*(c)* Baraza limefanya matayarisho ya ujenzi wa soko la Chuini ambapo mkandarasi kw aajili ya ujenzi ameshaptiakana na kazi za kuandaa michoro kwa ajili ya kuaza ujenzi zinaedelea.

**CHANGAMOTO ZINAZOLIKABILI BARAZA LA MJI MAGAHARIBI 'A'**

*(a)* Kutokuwepo kanzidata (database) ya uhakika kwa wafanyabiashara ambao wamesajiliwa na kutumika kwa Baraza kwa ajili ukusanyaji wa mapato.
*(b)* Kuwepo kwa uhaba wa vitendeakazi kama vile magari ya kuzolea taka na vifaa vyengine kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
*(c)* Kamati imebaini kuwepo kwa uelewa mdogo wa wananchi juu ya uhifadhi wa mazingira kulikotokana na elimu ndogo ya jamii katika kutunza mazingira.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Baraza lianzishe mfumo madhubuti wa kuwatambua wafanyabiashara wote ambao wanatumika kulipa kodi kwa lengo lamkutambua idadi yao na uwezo wao katika kulipa kodi.
*(i)* Baraza liandae mpango mkakati ambao utaliwezesha kununua vitendea kazi kupitia bajeti yake ya matumizi kwa kila mwaka wa fedha pamoja nakutumia mapato yake ya ndani.
*(ii)* Kamati inashauri Baraza linapofanya manunuzi ya vifaa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kununua vifaa ambavyo vinaubora na vinalingana na thamani ya fedha. Aidha, miradi inayotekelezwa izingatie matakwa ya wanannchi na mahitaji ya eneo husika.

## 3.12 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"

Baraza la Manispaa Magharibi 'B' limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji.

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI HALISI WA MAJUKUMU YA MANISPAA YA MAGHARIBI 'B'**

*(a)* Katika kuimarisha usafi wa mji, Baraza la Manispaa Magharibi "B" limezoa wastani wa tani 11,702 za taka ngumu kati ya tani 12,435 zilizokadiriwa sawa na asilimia 94 na kuzoa Majaa yasiyo Rasmi 12 katika maeneo ya Viwanda vidogovidogo, Magogoni kidatu, Skuli ya Magogoni Msingi, Mambosasa Angoza, Taveta/Uzi Mpakani,

Mwanakwerekwe Kivubo, Chukwani Mbuyuni, Taveta kwa Mzee Mtwana, Viwanja vya Magereza, Mshelishelini, Makaburi ya Wahindi na Kijitoupele.

*(b)* Baraza limeendelea kuimarisha shughuli za usafi katika maeneo ya barabarani, maeneo ya biashara na majumbani pamoja na kuimarisha bustani katika barabara ili kuleta haiba nzuri ya mji na kukagua jumla ya nyumba 148 katika Shehia ya Mwanakwerekwe, Tomondo, Kijitoupele na Kwarara ambapo nyumba 124 hazina makaro ya kuhifadhia maji machafu, na wafanyabiashara 129 wamekaguliwa na kupewa Elimu ya Afya pamoja na kutoa jumla ya matangazo 14 yanayohusiana na kazi za ofisi ikiwemo usafi.

*(c)* Baraza limehamasisha ukusanyaji wa Mapato kupitia vyombo vya habari na mikutano katika Shehia zote 34 kwa ajili ya kutoa elimu kwa Wananchi ili kuongeza uelewa na umuhimu wa ulipaji wa ada kwa wakati kupitia wakaguzi wa mapato ambapo kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2021 Baraza limekusanya jumla ya **Shilingi 869,185,737.**

*(d)* Jumla ya wajasiriamali 3,429 wamesajiliwa kutoka masoko ya Jumbi na Mwanakwerekwe na waliopatiwa vitambulisho ni 960. Serikali imeamua kutoa vitambulisho hivyo kwa wajasiriamali ili kutoa fursa mbali mbali ikiwemo mikopo na kutambulika kitaifa. Aidha, Baraza limefanya kipindi kimoja cha TV kinachohusiana na uhamasishaji wa uandikishaji wajasiriamali kwa kuwapatia vitambulisho ili waweze kutambulika Zoezi la kuwasajili wajasiriamali linaendelea ambalo limeanza mwezi Ogasti 2021 hadi sasa.

*(e)* Baraza limefanya matengenezo ya miundombinu ya umeme uwekaji wa tiles, vitasa, balb pamoja na kufanya makisio ya upakaji wa rangi katika jengo la ofisi na kuandaa makisio ya ujenzi wa uzio pamoja na Interlock katika jengo la ofisi.

*(f)* Katika kusimamia miundombinu ya masoko, ofisi imefanya matengenezo ya miundombinu ya maji machafu (chemba) na maji safi katika soko la Jumbi, imesimamia matengenezo ya maegesho ya Mwanakwerekwe pamoja kusimamia zoezi la uwekaji wa taa katika eneo la maegesho ya Kiembe samaki.

*(g)* Aidha katika usimamizi wa taa za barabarani ofisi imefanya marekebisho ya kuweka kufuli mpya katika vituo vitano vya umeme wa taa za barabarani na kurikodi namba za mita katika maeneo ya vituo hivyo ikiwemo Mombasa sokoni,

Mazizini eneo la vitambulisho, Mazizini kwa Mufti, Kwa mchina mwanzo pamoja na Kiembesamaki.

*(h)* Kwa upande wa maombi ya vibali vya ujenzi Ofisi imefanya ukaguzi katika maeneo tofauti yaliyoombewa vibali ndani ya Wilaya ya Magharibi 'B' ikiwemo Maungani, Fuoni, Chukwani, Kisauni, Magogoni, Dimani, Mwanakwerekwe, Mombasa, Kisakasaka na Mitondooni hivyo maeneo yote hayana tatatizo pamoja na kutoa muongozo wa ujenzi. Vilevile ofisi ilikusanya Jumla ya **shilingi 24,265,000/=** kupitia akaunti ya D.C.U na Jumla ya vibali 95, pamoja na marejeo 9 vilitolewa kwa ajili ya ujenzi.

*(i)* Baraza kupitia kitengo cha Sheria limekabidhi kanuni za kudumu za uendeshaji wa Mabaraza kwa Waheshimiwa Madiwani wa Baraza la Manispaa Magharibi 'B' pamoja na Rasimu ya kanuni za papo kwa papo na Ushuru wa Huduma, katika makabidhiano hayo kitengo kimeeleza kwa muhtasari juu ya kanuni zote zilizotungwa pamoja na hatua zilizofikia hadi sasa. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2021 kitengo cha Sheria kimefanikiwa kusimamia kesi 6 zilizowasilishwa katika Ofisi zikiwemo kesi za kukata miti bila ya kibali, kuzurura ovyo kwa wanyama kama ng'ombe ndani ya Manispaa ya Magharibi "B" kesi za wanaotiririsha maji ovyo kwa kutokuwa na karo.

*(j)* Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2021 Baraza la Manispaa Magharibi "B" lilikadiria kukusanya **Shilingi 730,300,000** na limefanikiwa kukusanya **Shilingi 869,185,737** sawa na **asilimia 119** kutoka vyanzo vya ndani. Moja ya sababu ambazo zimepelekea kupanda kwa mapato ni kuongezeka kwa chanzo cha mapato ambacho ni soko la Mwanakwerekwe sambamba na jitihada na usimamizi wa wafanyakazi wa mapato wakishirkiana na Wahasibu, na Mipango kwa kuwasimamia wakusanyaji wa mapato katika kazi zao za kila siku.

**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI 'B'**

Licha ya mafanikio kadhaa yaliyofikiwa na Baraza la Manispaa Magharibi 'B' kutokana na utendaji kazi wao ambao hauna shaka umefanyika kwa mujibu wa sharia nataratibu za Manispaa, pia zipo changamoto ambazo zikipatiwa ufumbuzi maendeleo zaidi yataweza

kufikiwa katika Baraza la Manispaa hii. Miongoni mwa changamoto hizi ni kama ifuatavyo:-

*(i)* Kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya kuzolea taka namashine za kisasa za ukusanyaji wa mapato.
*(ii)* Uelewa mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa kodi pamoja kutofanya malipo kwa wakati.
*(iii)*Ukosefu wa mipango miji ambao unakwaza zoezi la usafi na kusababisha kuenea kwa taka katika maeneo ya miji.
*(iv)*Ujenzi holela katika maneo hatarishi ambayo huathirika kwa maji wakati wa mvua kubwa na hivyo kupelekea baadhi ya wananchi kuhama makaazi yao wakati wa mvua kubwa za masika.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Kwa kuwa Kamati imeridhishwa na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa majukumu ya Baraza kwa kipindi hiki, pia haikusita kushauri mambo mbali mbali ambayo kimsingi yanadhamira ya kuimarisha maendeleo ya Manispaa Magaharibi 'B' kwa hivyo, miongoni mwa mambo ambayo Kamati inashauri ni kama ifuatavyo:-

*(i)* Baraza lizidishe kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kuvitumia vyema vyanzo vyake vya mapato na kwa mujibu wa taratibu wa kisheria bila ya kuwaonea wafanyabishara na wajasiriamali wadogo wadogo.

*(ii)* Baraza liandae mpango mkakati ambao utasaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa vitendea kazi ikiwemo magari ya taka ili kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa taka katika mji.

*(iii)*Baraza litoe elimu kikamilifu kupitia vyombo vya habari na mikutano na wanajamii juu ya umuhimu usafi wa mazingira na lisisite katika kuwachukulia hatua wale wote wanaochafua mazingira na kuhatarisha maisha ya wananchi.
*(iv)*Baraza liongeze kasi ya mashirikiano baina yake na waheshimiwa Madiwani kwa kuwapatia stahiki zao kikamilifu na kuwashirikisha katika ngazi zote za kimaendeleo kupitia miradi inayotekelezwa katika Baraza.

## 3.13 OFISI YA MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mkoa wa Kusini Unguja umeundwa kwa mujibu wa Sheria nambari *8* ya Tawala za Mikoa ya mwaka *2014.* Mkoa unatekeleza majukumu yafuatayo: kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI HALISI WA MAJUKUMU YA MKOA WA KUSINI UNGUJA:**

Katika utekelezaji wa majukumu ya Mkoa wa Kusini Unguja yamebainishwa katika sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 kama ilivyo kwa Mikoa mengine ya Zanzibar. Miongoni mwafanikio yaliyopatikana kwa kipindi hiki ni haya yafuatayo:-

*(a)* Mkoa umefanikiwa kusimamia hali ya ulinzi na usalama wa Mkoa kwa kuendelea kuimarisha amani na utulivu kwa wananchi ambapo vikao 30 vya Kamati za Usalama Mkoa na Wilaya vimefanyika vikiwemo vya dharura 13 na kawaida 17 kwa lengo la kuweka mikakati mbali mbali ya kuimarisha amani na usalama.

*(b)* Kuwepo kwa mapambano dhidi ya dawa za kulevya, ajali za barararani na matukio ya moto; elimu imetolewa katika Shehia 36 pamoja na kusikiliza kero na changamoto za wananchi. Aidha, malalamiko 81 ya ardhi yaliripotiwa, kati ya hayo 27 yamepatiwa ufumbuzi, 16 yamepelekwa Mahakamani, 5 Kamisheni ya Ardhi na 33 yanaendelea na hatua za utatuzi katika ngazi ya Wilaya.

*(c)* Mkoa umefanikiwa kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na Utekelezaji wa maagizo ya viongozi kupitia ziara ya Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na kutembelea maeneo ya miradi iliopo Mkoa wa Kusini ambapo maelekezo na maagizo 12 yametolewa na ufayiwa kazi.

*(d)* Mkoa umefanikiwa kutoa huduma za kiutawala na uendeshashaji kwa kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ambapo wafanyakazi 5 wanaendelea na

mafunzo ya muda mrefu na 31 wamepatiwa mafunzo ya awali (induction course).

## 3.14 BARAZA LA MJI KATI

Mafanikio yyaliyopatikana katika Utekelezaji wa Baraza la Mji Kati, nika yafuatayo:

*(a)* Kuweka mikakati imara ya kuimarisha mradi wa usafi wa mazingira, ikiwemo kufunga mkataba wa kusimamia usafi katika Shehia na kukabidhi vifaa vya usafi kwa kikundi cha Vijana wa Tunguu (Tunguu Enhencement).

*(b)* Kuingia mkataba na Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Dunga Kiembeni na taratibu za ujenzi zinaendelea pamoja na kusafisha eneo la Kikungwi na Pete kwa ajili ya ujenzi wa masoko.

*(c)* Kuwajengea uwezo wajasiriamali na makundi maalum kwa kukamilisha mradi wa kilimo na mifugo kwa ushirika wa vijana uliopo Hanyegwa ambao umejumuisha *green house,* pamoja na mabanda mawili ya mifugo ya kuku na Sungura. Aidha, zoezi la ushajihishaji na usajili wa Wajasiriamali wadogo wadogo wa Wilaya ya Kati linaendelea hadi kufikia Disemba, 2021 jumla ya wajasiriamali 1,196 wamesajiliwa na 359 Wamekamilisha Taratibu za malipo na waliopatiwa Vitambulisho vyao ni 121.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BARAZA LA MJI KATI**

Katika hatua ya mafanikio yaliyopatikana na kupiga hatua ya maendeleo, Baraza la Mji Kati linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa watendaji.
*(ii)* Mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa kiasi kikubwa yamewaathiri wakulima na wajasiriamali.
*(iii)* Uelewa mdogo wa wafanyabiashara katika kulipa kodi na kutumia mashine za ukusanyaji wa mapato.
*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ukusanyaji wa mapato ambpo kwa kipindi cha Oktoba – Disemba, 2021 ni asilimia 55 tu ya mapato yaliyokusanywa katika makadirio ya Baraza.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

Ili kuweza kufikia hatua ya mafanikio katika Baraza la Mji Kati na kufikia hatua iliyokusudiwa, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

*(a)* Kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutoa elimu kwa wafanya bishara pampoja na kubuni vyanzo vipya vitakavyosaidia ongezeko la mapato.

*(b)* Baraza liwafikie wajasiriamali wadogo wadogo na kutatua changamoto zao ambazo zinarudisha nyuma maendeleo yao. Aidha, fungu maalumu la mapato kwa ajili ya makundi maalumu litiliwe mkazo ili kuwasaidia walengwa.

*(c)* Kamati inashauri suala la usafi wa mji kuongezewa bidii na kuhakikisha kila mmoja katika jamii amewajibika kwa eneo lake katika kuweka mazingira safi na salama.

## 3.15 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja ni kama yafuatayo:

*(a)* Kuimarisha usafi wa mazingira. Halmashauri imeendelea kufanya usafi katika maeneo yote ya Wilaya ya Kusini kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali kama vile SUZA, ZANREC, ZATU, CHAVIZA na Kamati ya Tamasha la Kizimkazi. Aidha, Halmashauri inaendelea kuimarisha usafi katika maeneo mbali mbali kwa kuzoa taka katika maduka na Hoteli zilizowekwa ndoo za kuhifadhia taka ambapo jumla ya tani 1026.122 za taka zilizolewa na kutupwa katika jaa kuu Kibele.

*(b)* Kuwawezesha wajasiriamali. Halmashauri inaendelea na zoezi la kuwasajili Wajasiriamali kwa kipindi cha Oktoba – Disemba, 2021 ambapo jumla ya wajasiriamali 407 wamesajiliwa kati ya hao ni wajasiriamali 36 wamelipia na kupatiwa vitambulisho. Aidha, katika kuwajengea Wajasiriamali maeneo ya kudumu ya kufanyia biashara Halmashauri imemalizia ujenzi wa soko la Makanduchi kwa hatua ya sakafu, rangi na milango ambapo jumla ya Shilingi 5,600,439.6 zimetumika.

*(c)* Katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Halmashauri ilipanga kukusanya Shilingi 160,456,994 katika kipindi cha miezi sita na imefanikiwa kukusanya Shilingi 173,012,754 sawa na asilimia 107.82

**CHANAGMOTO ZINAZOIKABILI HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA:**

Kamati utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja, imeweza kukabiliwa na mambo yafutayo:-

*(i)* Uhaba vitendea kazi vya kisasa katika ukusanyaji wa mapato.

*(ii)* Uelewa mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa mapato na kulinda vyanzo vya mapato.

*(iii)* Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa watendaji wa Halmashauri.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA**

*(i)* Kamati inaipongeza sana Halmashauri hii kwa kuvuka malengo yake katika ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miezi 6, hivyo, juhudi zaidi zinahitajika katika kuibua vyanzo vipya vitakavyo ongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato.

*(ii)* Kamati inashauri elimu zaidi itolewe kwa wajasiriamali wadogo wadogo ili kuwasaidia wakati wa kubuni miradi yao na kutoshindwa kufikia malengo.

*(iii)* Halmashauri isimamie wajasiriamali kuweza kupata vitambulisho na kuwasajili wote kuwatambua kama inavyoelekezwa katika taratibu za kitaifa.

**3.16 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA**

Mkoa wa Kaskazini Unguja umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na

usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

Mkoa wa Kaskazini Unguja unajumla ya Wilaya mbili; Wilaya ya Kaskazini "A" na Wilaya ya Kaskazini "B" pamoja na Halmashauri za Mabaraza ya miji; Baraza la Mji Kaskazini "A" na Baraza la Mji Kaskazini "B".

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Taifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ilifanikiwa kutembelea Baraza la Mji Kaskazini A na Braza la Mji Kaskazini B Unguja.

## 3.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI "A"

Baraza la Mji Kaskazini "B" Unguja ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja yalioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa, uwezo wake, kazi na wajibu, muundo, mpangilio, fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA BARAZA LA MJI KASKAZINI "A"**

*(a)* Kusimamia suala la usafi ambapo jumla ya ziara 26 za usafi zimefanyika kwa kipindi cha Oktoba – Disemba,2021 na kufanya ukaguzi kwa mama/baba lishe 113 pamoja na kuwachukulia hatua waliobainika kukiuka kanuni za kiafya na kufanya mazoezi 20 ya usafi katika maeneo tisa. Aidha, Baraza limeendelea na zoezi la usafi kwa kila siku ya jumamaosi ya kila wiki katika maeneo ya Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja.

*(b)* Katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Baraza limeimarisha maegesho ya magari Mkokotoni na kujenga vyoo katika eneo hilo, kujenga ghala moja na milango saba ya maduka. Aidha wananchi wanane (8) wamelipwa fidia kwa ajili ya kupisha ujenzi wa soko la Kinyasini pamoja na kufanya malipo ya deni la vifaa vya ujenzi vilivyotumika katika ujenzi wa nyumba ya daktari Pwani mchangani.

*(c)* Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, kwa kipindincha Oktoba – Disemba, 2021 Baraza limefanya ziara tisa (9) za

ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato katika vituo 17 ndani ya wilaya na kufanya mikutano miwili (2) ya wananchi kwa lengo la kuwahamasisha juu ya ulipaji wa ada na tozo.

**CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELZAJI WA BARAZA LA MJI KASKAZINI "A" UNGUJA:**

Licha ya mafanikio mbali mbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa Baraza la Mji Kaskazini 'A' Unguja, pia zipo changamoto ambazo hurudisha nyuma maendeleo yao, mmiongoni mwa changamoto hizo:-

*(i)* Uhaba wa vyombo vya usafiri katika uendeshaji wa shughuli za Baraza; matokeo yake ni kushindwa kufuatilia vyema katika vyanzo vya mapato na miradi ya maendeleo.
*(ii)* Uhaba wa watumishi katika fani mbali mbali ikiwemo wataalamu wabunifu katika masuala ya mapato.

*(iii)* Kamati imebaini kuwepo kwa mashirikiano madogo baina ya Baraza na wananchi katika kuibua miradi ya maendeleo. Suala hili limepelekea wananchi kutounga mkono juhudi za ujenzi wa soko la samaki Mkwajuni na hivyo kusababisha malalamiko ya kila siku kwa wananchi.

*(iv)* Kamati pia, imebaini kuwepo kwa changamoto ya kuchelewa kufanywa malipo ya wafanyakazi wa mkataba, jambo ambalo linanyima ari na hamasa ya ufanyaji kazi kwa watumishi hawa.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Kutokana na changamoto mbali mbali ambazo Kamati wamezibaini na kuzitolea ufafanuzi wakati wa ziara zake; hata hivyo, Kamati inaendelea kushauri mambo yafuatayo:-

*(a)* Kamati inalishauri Baraza kuzingatia ushauri wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwashirikisha kikamilifu katika kuibua na kutekeleza miradi hiyo kwani walengwa wa miradi hiyo ni wananchi wenyewe.

*(b)* Kamati inalishauri Baraza kutenga bajeti yake maalumu kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri katika utekelezaji wa shughuli zake.

(c) Baraza lihakikishe linalipa maposho ya wafanyakazi wa mkataba kwa wakati ili kuepusha kufanyika udanganyifu katika ukusanyaji wa mapato.

(d) Kamati inashauri miradi inayoibuliwa na Baraza ikamilishwe kwa wakati na ijengwe katika kiwango kinachofaa kwa kuwasimamia vyema wataalamu wa miradi hiyo. Vile vile, miradi ifanywe kwa kuzingatia mgawanyo wa Wadi zilizomo katika Baraza.

(e) Kamati pia, inalishauri Baraza kuwashirikisha vyema waheshimiwa Madiwani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kulinda heshima na maslahi ya Madiwani katika Nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

## 3.18 BARAZA LA MJI KASKAZINI "B"

Baraza la Mji Kaskazini "B" Unguja ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja yalioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa, uwezo wake, kazi na wajibu, muundo, mpangilio, fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Baraza la Mji Kaskazini "B" linasimamiwa na Baraza la Madiwani linaloongozwa na Mwenyekiti wa Baraza. Baraza lina jumla ya Madiwani 15 ambao kati yao, Madiwani 7 ni wa kuchaguliwa kutoka katika Wadi, Madiwani 3 wanatokana na Viti Maalum na Madiwani 5 ni wakuteuliwa na Mhe. Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

### MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA BARAZA

Katika utekelezaji wa shughuli za Baraza mafanikio mbali mbali yamepatikana katika kipindi cha utekelezaji, kama ifuatavyo:-

(a) Kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii, ikiwemo kuwapatia taaluma wananchi juu ya usafi wa mazingira na ulipaji wa ada kwa hiari na kuwapatia huduma kwa wakati.

*(b)* Baraza limefanikiwa kuwasajili wajasiriamali wadogowadogo 485 kwaajili kuwapatiwa vitambulisho katika shehia 31 za Wilaya ya Kaskazini 'B'.

*(c)* Katika kuongeza wigo wa mapato Baraza la Mji Kaskazini 'B' limelazimika kufanya ufuatiliaji katika vyanzo vya mapato mpaka siku za mapumziko kuhakikisha linaongeza makusanyo.

*(d)* Kuendelea kukusanya mapato kwa mfumo wa elektroniki pamoja na kukamilisha hatua za maandalizi za utoaji leseni kupitia mfumo mpya wa Serikali wa utoaji lesseni kwa mtandao ili kuongeza ufanisi katika kusanyaji wa mapato.

*(e)* Kuongeza vitendea kazi vya kukusanyia mapato vya kielektroniki ikiwemo POS mashine pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji ili kuwa tayari kutoa msaada kwa Wananchi wakati mfumo utakapoanza kutumika rasmi.

**CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, pia zipo changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za Baraza, miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

*(a)* Kutopatiwa mgao stahiki na kuchelewa kwa mapato yatokanayo na rasilimali ya mchanga.

*(b)* Kuondoshwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kupelekwa Serikali kuu.

*(c)* Kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri katika kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika vyanzo vya mapato.

*(d)* Kuwepo kwa uelewa na mwamko mdogo wa wananchi katika kutumia mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato na usajili wa wajasiriamali.

*(e)* Kukosa mapato kutoka chanzo cha minara ya simu kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa wataalamu wa ukusanyaji wa mapato.

*(f)* Kamati imesikitishwa na Baraza hili kuona mpaka sasa suala la ukusanyaji wa taka halijafanyiwa kazi ipasavyo, jambo ambalo ndio jukumu la msingi kwa mabaraza.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

Katika kukabiliana na changamoto hizo juhudi na mikakati mbalimbali inahitajika ili kuona changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua. Hivyo, basi Kamti inashauri kama ifuatavyo:-

*(a)* Kutokana na kupungua kwa ukusanyaji wa mapato, Baraza la Mji Kaskazini 'B' liendelee na kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitasaidia kuongeza mapato na kuacha kutegemea chanzo kimoja cha mchanga.

*(b)* Katika kuhakikisha wananchi wanapata uelewa mzuri juu mfumo mpya wa ukusanyaji na udhibiti wa mapato, Baraza la Mji liendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa matumizi za mashine za ukunyaji wa mapato.

*(c)* Baraza liandae mpango maalum wa rasilimali watu utakaowezesha kufahamu mapungufu ya wataalamu yaliyopo katika Baraza ambapo ni pamoja na wataalamu wa ukusanyaji wa mapato.

*(d)* Baraza lihakikishe linalinda maslahi ya Madiwani pamoja na kutekeleza miradi kwa kuzingatia uwiano wa Madiwani na kuwashirikisha katika upangaji wa miradi na matumizi.

## 3.19 OFISI YA MKOA WA KUSINI PEMBA

Mkoa wa Kusini Pemba umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

## 3.20 OFISI YA MKUU WA MKOA KUSINI PEMBA.

***Utekelezaji halisi wa shughuli zilizopangwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba:***

1. **Kuimarisha hali ya ulinzi na usalama katika mkoa wa kusini Pemba.**
   Katika kusimamia hali ya ulinzi na Usalama wa Mkoa mambo mbali mbali yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na kuendeleza amani na utulivu, udhibiti wa dawa za kulevya, matukio ya udhalilishaji wa kijinsia, udhibiti wa utoro wa wanafunzi shuleni, udhibiti wa biashara za Magendo ya Karafuu. Kufatia vikao hivyo mikakati mbali mbali yakupambana na matukio hayo iliandaliwa.

2. ***Utekelezaji wa mpango mkakati wa kitaifa juu ya kupambana na masuala ya udhalilishaji Mkoa wa Kusini Pemba.***
   Mkoa kwa kushirikiana na wadau mbali mbali umesimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kitaifa wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na ambapo elimu juu ya kupambana na udhalilishaji imetolewa kwa shehia tano (5) na kamati za skuli saba (7) za msingi kwa lengo la kuhamasisha mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na ufuatiliaji wa matukio ya udhalilishaji ambapo jumla ya matukio 82 ikiwa ni pamoja na udhalilishaji, mvutano wa malezi pamoja na watoto wanaokinzana na malezi yameripotiwa.

3. ***Utoaji wa huduma za utumishi na uendeshaji Mkoa Kusini Pemba.***
   Katika kutekeleza Programu ya Utawala na Uendeshaji, Mkoa umeweka mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi stahiki. Mbali na hayo, Ofisi iliawapatia wafanhyakazi stahiki zao ikiwa ni pamoja namalipo baada ya saa za kazi wafanyakazi 10, likizo wafanyakazi 13, posho la kujikimu na malazi wafanyakazi 16.

### CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MKUU WA MKOA KUSINI PEMBA.

Pamoja na mafanikio yaliopatikana katika utekelezaji wa majukum yao ya kila siku bado kuna changamoto ndogo ndogo ambazo Kamati

imezibaini na zinafaa kuchukuliwa hatua. Changamoto hizo ni kama zifuatazo: -

*(i)* Uchakavu na ufinyu wa majengo ya Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya – ChakeChake na Mkoani.

*(ii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika Ofisi za Wilaya.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI.**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango maalumu utakaowezesha wakuu wa Wilaya na Mikoa kupata makaazi bora kwa kuzikarabati nyumba wanazoishi au kujengwa mpya pale ambapo uwezo utaruhusu.

*(ii)* Kamati pia, inaiomba Serikali kuwapatia watendaji wa ofisi za Wilaya na Mkoa vifaa vya kazi ikiwemo vyombo vya usafiri ili kuimarisha mazingira yao ya kazi.

*(iii)* Kamati inashauri watendaji wa Mkoa kuzidisha kasi ya utendaji ili kumsaidia Mkuu wa Mkoa kwa kutoa huduma bora katika jamii.

## 3.21 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE.

***Utekelezaji halisi wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Baraza la Mji Chake – Chake:***

1. ***Huduma za uendeshaji na Kuwajengea uwezo wafanyakazi;*** Kwa upande wa kuwaendeleza wafanyakazi, ofisi imelipia mafunzo kwa wafanyakazi wapya 21 (induction course) (Shs1,000,000/=) na pia kumlipa mfanyakazi mmoja aliyesomea mafunzo ya udereva huko Dar-es Salaam (Shs 500,000/=). Ofisi imetoa huduma za uendeshaji ikiwa ni pamoja na matengenezo ya vifaa, na mafuta ya uendeshaji, malipo ya huduma ikiwemo maji, umeme, internet, pamoja na kufanya matengenezo ya vyombo vya moto na kufanya ufuatiliaji wa kazi za kila siku.

2. ***Kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo ya Miji;*** Katika kipindi cha Julai-Septemba Baraza la Mji Chake Chake limefanikiwa kukusanya tani za taka ngumu 1274

pamoja namitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 2300 ilisafishwa, Baraza linaendelea kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya Miji ya Chake Chake pamoja na kusafisha mitaro ya maji ya mvua.

3. ***Kuyawezesha makundi maalum kuimarika kiuchumi;***
Kupitia programu ya kuwawezesha vijana, wajariamali na makundi maalum kuimarika kiuchumi – Ofisi imetenga jumla ya T.Shs 12,975,000/= kutumika baada ya Ofisi kupata muongozo kutoka Serikali kuu kuhusiana na utaratibu wa kuziwasilisha fedha hizo kwa walengwa.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE**

Pamoja na kuimarika kwa hali ya usafi wa Mji kwa kufikia shehia nyingi zaidi Ofisi ya Baraza la Mji Chake chake inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadha wa kadha ambazo zinarudisha nyuma maendeleo ya Mji na Vitongoji vyake. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatavyo:-

1. Tatizo la Mtandao katika shughuli za ukusanyaji mapato.
2. Uhaba wa mashine za kukusanyia mapato.
3. Ubovu wa gari la maji taka.
4. Uhaba na uchelewaji wa fedha za OC.
5. Kukosekana kwa sehemu ya jaa kuu linaloendana na wakati.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI.**

*(i)* Kamati inashauri Baraza kufanya juhudi za makusudi kutafuta mtaalamu atayeboresha mfumo wa mashine za ukusanyaji wa mapato ili kuzuia mianya ya upopteaji wa mapato. Aidha, ni vyema kama Baraza likiwa na mataalamu wake wenyewe ambaye atatumika kufanya marekebisho kila atakapo hitajika.

*(ii)* Kamati inaishauri Serikali ya Mkoa kusaidia Baraza kupata eneo litakalo tumika kama jaa kuu na kupunguza kuenea kwa takataka hovyo hovyo mitaani.

*(iii)* Baraza pia, lijikite katika usafi wa mji, ukusanyaji wa mapato na kutoa huduma kwa jamii kwani hizo ndio kazi kuu za Mabaraza na Halmashauri.

*(iv)*Kamati inashauri Baraza kulinda na kusimamia maslahi ya waheshimiwa Madiwani katika shughuli zao za kila siku ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha katika miradi inayoibuliwa katika maeneo yao.

*(v)* Kamati inasikitishwa na namna Baraza linavyotekeleza miradi yake kwa kuangalia upande mmoja huku wakiachwa baadhi ya Madiwani wakikosa miradi katika Wadi zao, jambo ambalo litawaathiri hapo baadae.

## 3.22 BARAZA LA MJI MKOANI-PEMBA.

***Utekelezaji halisi wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Baraza la Mji Mkoani:***

1. **Kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya Mji;**
   Kwa kipindi kifupi, Baraza limefanikiwa kufanya usafi wa mji ambapo jumla ya tani za taka 288 zimezolewa na kutupwa katika jaa kuu la Chokaani, sambamba na kusafisha misingi mitatu ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 1.2 ikiwemo Mikarafuuni-Mpika tango, Msikiti wa Ijumaa-Mpika tango, na Makadara-Ng'ombeni pamoja na kuimarisha upandaji wa bustani katika maeneo ya Mji.

2. **Kulipa stahiki za wafanyakazi kwa wakati;**
   Baraza la Mji Mkoani limefanikiwa kulipa stahiki za wafanyakazi ikiwemo mishahara kwa wafanyakazi pamoja na posho la safari kikazi kwa wafanyakazi 7 na Mjasiriamali mmoja aliyeshiriki katika uzinduzi wa vitambulisho vya wajasiriamali Unguja.

3. **Kuyawezesha makundi maalum kuimarika kiuchumi;**
   Katika programu ya kuwawezesha vijana, wajariamali na makundi maalumu kuimarika kiuchumi, Ofisi imetenga jumla ya T.Shs 5,094,585/= kutumika, baada ya ofisi kupata muongozo kutoka Serikali kuu kuhusiana na utaratibu wa kuziwasilisha fedha hizo kwa walengwa.

**_CHANGAMOTO_ ZINAZOIKABILI BARAZA LA MJI MKOANI.**

Licha ya Baraza kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa ufanisi na uwazi zaidi lakini bado kuna changamoto mbali mbali zinazoikabili katika kufanikisha shughuli zake, miongoni mwa Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Uhaba wa upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo ukilinganisha na mahitaji yaliyopo.

(ii) Ufinyu wa Ofisi ukilinganisha na wafanyakazi waliopo ambapo hulazimika kila chumba kutumiwa na wafanyakazi zaidi ya wawili.

(iii) Uhaba wa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri na gari la taka pia ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza.

(iv) Kuwepo kwa chinjio la ng'ombe ambalo halitumiki kwa kawaida na badala yake wanyama kuchinjwa mbali na chinjio liliowekwa kisheria.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

(i) Katika ujenzi/ukarabati uliofanywa katika Ukumbi wa Umoja ni Nguvu wa Mkoani; Kamati haikuridhishwa na hali tuliyoiona kwani usanifu uliofanywa ndani ya ukumbi haukuzingatia utaalamu na hivyo kuleta sura mbaya kwa Taasisi kama hii.

(ii) Kamati inalishauri Baraza kutekeleza miradi ambayo imo katika mipango na bajeti ya Baraza badala ya kufanya miradi ambayo haikupangwa na Baraza au kupitishwa kwa makubaliano na Kamati ya Fedha.

(iii) Kamati pia, inashauri Baraza kuangalia upya watendaji waliopo katika majengo ya ofisi na ambao hawahusiki na ofisi za Baraza basi ni vyema kuondolewa ili kutoa nafasi kwa watendaji wake.

(iv) Kwa namna yoyote ambayo itachukuliwa na Baraza ni lazima kuwepo kwa vifaa vya usafi kwani usafi ndio jukumu la msingi kwa Baraza. Hivyo, Kamati inashauri katika Bajeti inayokuja kuhakikisha kumetengwa fungu maalumu la ununuzi wa vifaa vyote vya usafi ili kutimiza wajibu huu katika mji wetu.

## 3.23 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mkoa wa Kaskazini Pemba umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na

usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

Mkoa wa Kaskazini Pemba umeunganishwa na Wilaya Mbili (2), Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni pamoja na Wilaya ndogo ya Kojani. Ongezeko la watu kwa mwaka ni 3.3% Mkoa huu, una Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya yenye Majimbo 9 ya Uchaguzi, Wete 5 na Micheweni 4, Wadi 18 na Shehia 61.

***Utekelezaji wa Mkoa wa Kaskazini Pemba***

1. ***Kuimarisha hali ya ulinzi na usalama Mkoa.***
   Mkoa umeendela kuratibu vikao mbali mbali kwa lengo la kujadili na kusisitiza masuala ya kuimarisha Amani na Usalama katika Mkoa, Ukodishwaji wa mashamba ya Mikarafuu, Kujadili na kuyapitisha Majina ya Vijana wa ajira za Polisi na Uhamiaji, Udhibiti wa bidhaa za Magendo ikiwa ni pamoja na Magendo ya Karafuu, Udhibiti wa vitendo vya wizi wa mazao na mifugo, Udhibiti wa Dawa za kulevya pamoja kudhibiti vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto.

2. ***Kupambana na masuala ya udhalilishaji Mkoa.***
   Juhudi mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Viongozi wa Mkoa na Wilaya ili kupambana na kudhibiti vitendo vya Udhalilishaji, jumla ya shehia 17 za wilaya wa Wete na Micheweni zilipatiwa elimu ya masuala ya udhalilishaji pamoja na Skuli za Msingi, Sekondari na madrasa za Qur-ani ili waweze kuepukana na Vishawishi na viashiria vinavyo pelekea udhalilishwaji miongoni mwao.

*Malalamiko ya udhalilishaji yaliripotiwa:*

| S/no | AINAYA TUKIO | Idadi | Ke | Me | Jumla | hatua iliyofikia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Kubaka | 14 | 14 | 0 | 14 | 4-ziko mahakamani, 10-upelelezi Polisi |
| **2** | Shambulio la aibu | 06 | 06 | 0 | 06 | Ziko Polisi kwa upelelezi |
| **3** | Kutorosha | 02 | 02 | 0 | 02 | Ziko polisi |
| **4** | Kumuingilia mgonjwa wa akili | 01 | 01 | 0 | 01 | 1-imetolewa hukumu na ziko mahakamani. |
| 5 | Kunajisi | 01 | 01 | 0 | 01 | 1Iko polisi |
| 6 | Utelekezaji | 07 | 03 | 04 | 07 | zote- zimepatiwa Suluhu, katika ngazi ya Wilaya. |
| 7 | Mvutano wa malezi | 04 | 02 | 02 | 04 | Zote-Zimepatiwa suluhu Wilayani. |
| | **JUMLA** | **34** | **28** | **06** | **34** | |

*Jaduweli nambari: 1. Matokeo mbali mbali ya udhalilishaji katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.*

3. ***Utoaji wa huduma za afya:***
   Kwa upande wa huduma za Afya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba imefanikiwa kuratibu shughuli za makabidhiano ya vifaa tiba kwa hospitali ya Wete vilivyotolewa na wahisani wa maendeleo Vifaa vilivyokabidhiwa ni pamoja na vitanda vya kujifungulia waja wazito 3 magodoro 5 kiti cha kubebea wagonjwa kimoja 1, mashine ya kupimia mapigo ya moyo, mashine ya kuchunguzia magonjwa mbalimbali (Micro Scope) Sare za wafanyakazi, vitanda vya kuhifadhia watoto wanaozaliwa kabla ya muda (watoto njiti) Mashine za kuekea Oxygen (2) B.P Monitor 6, Cardial Table(2) Neck Support (12) na vyengine vingi.

4. ***Uboreshaji wa mifumo ya elimu:***
   Kamati inapongeza uongozi wa Mkoa kwa kukutana na Walimu wakuu wa Skuli zote za Mkoa ili kujadili na kupanga mikakati ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wetu wameweza kufanya itihani yao kwa Utulivu na kuboresha mazingira yao ya kujifunzia ili kupata ufaulu unaolingana na malengo ya Serikali.

Aidha, katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku; Kamati imebaini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba inakabiliana na changamoto zifuatazo:-

1. Ufinyu wa afisi kulinganisha na idadi ya wafanyakazi.
2. Ufinyu wa Bajeti kutokana na mahitaji ya afisi.
3. Uhaba wa fedha za Matumizi Maalumu ya Mkuu wa Mkoa kulingana na mahitaji ya Wananchi (Political Vote)

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Kamati inashauri kutekeleza mpango wake wa kuongeza eneo (partition) la ofisi kwa baadhi ya vyumba vyenye nafasi ili kupata nafasi zaidi.

*(ii)* Kuhusu suala la bajeti, Kamati inashauri Ofisi kufanya maombi kwa kufuata utaratibu maalumu wa maombi na kuyawasilisha katika wizara husika ili kupata nyongeza ya badget.

*(iii)* Kamati pia, inaishauri Serikali kuongeza fedha za matumizi maalum (Political Votes) kutokana na kiwango kidogo kilichopo ambacho hakikidhi mahitaji ya wananchi.

## 3.24 OFISI YA MKUU WA WILAYA WETE

**Utekelezaji wa Shughuli za Wilaya:**

*(a)* **Jitihada za kuthibiti wizi wa mifugo na mazao**;
Katika kudhibiti wizi wa mifugo na mazao, Wilaya inafanya operesheni maalumu kwa ajili ya kudhibiti wizi wa mifugo na mazao, katika operesheni hizo Wilaya imefanikiwa kukamata kuku 32 katika Shehia ya Kisiwani, na matukio 10 ya wizi wa mifugo yameripotiwa kati ya hayo matukio saba yanaendelea na upelelezi, moja liko Mahkamani, moja liko kwa DPP na moja limefungwa.

***(b)*** **Ufumbuzi wa kesi za migogoro ya ardhi.**
Kwa kipindi cha July – Septemba 2021, jumla ya migogoro 6 ya ardhi imeripotiwa na kupatiwa ufumbizi wa kina katika kipindi tajwa kutoka shehia ya Shengejuu, Pandani, Mtambwe Kaskazini na Limbani

***(c)*** **Ufumbuzi wa kero za wananchi.**

Kamati inapongeza juhudi za Wilaya kuanzisha mpango wa kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia Ufumbuzi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika kijiji cha Taifu Shehia ya Kinyasini, uboreshaji wa huduma ya maji safi na salama kijiji cha Kilimahewa Shehia ya Mtemani, Maungweni Shehia ya Kiuyu Minungwini, Miti miwili Shehia ya Kizimbani na Masota Shehia ya Shengejuu, Wilaya ilisimamia ujenzi wa madarasa mawili skuli ya Makongeni msingi, kuezeka vyumba nane skuli ya Jadida na vumba vitano Skuli ya Mgogoni.

***Mafanikio yaliyopatikana katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Wete.***

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni:-

1. Kuongeza kasi ya kusaidia vikundi vya wajasiriamali vikiwemo vikundi vya vijana, Wanawake na Watu wenye ulemavu;

2. Kuongezeka kwa watoto waliorudi mashuleni ambao walikua tayari wameshatoroka kutokana na sababu mbali mbali;
3. Kuongezeka kwa usajili wa vikundi vya ushirika ambavo vitatoa fursa kwa wananchi katika kujikwamua na umasikini.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*1.* Kamati inashauri uongozi wa Wilaya kusimamia kikamilifu maendeleo ya wajasiri amali pamoja na watu wa makundi maalumu ili kufikia malengo ya Serikali katika kupunguza umasikini.

*2.* Kamat inashauri vikundi vinavyoanzishwa kusimamiwa kwa kupewa nyenzo za kazi au mitaji ya kibiashara ili kuinusuru jamii kushiriki katika vitendo viovu.

## 3.25 OFISI YA MKUU WA WILAYA MICHEWENI

***Utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa:***

***(a)*** **Kusimamia hali ya Ulinzi na Usalama kwa Wilaya ya Micheweni.**
Uongozi wa Wilaya ulikutana na kujadili usalama wa wilaya kwa kuangalia bandari Bubu, udhibiti wa magendo ya karafuu, mapambano dhidi ya dawa za kulevya na mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

***(b)*** **Kuthibiti wizi wa Mifugo na mazao Wilaya ya Micheweni.**
Katika Kupinga vita suala la wizi wa Mifugo na Mazao ya Wafugaji na wakulima, Wilaya imeendelea kutekeleza agizo hilo kwa kuzungumza na masheha wote ili kuhakikisha wanatoa vibali vya mazao wakati wa usafirishaji wa mazao na mifugo pamoja na kuliagiza Jeshi la Polisi kusimamia hilo kwa kupekua gari zote zinazosafirisha mifugo na mazao.

***(c)*** **Kuratibu na kufatilia shughuli mbali mbali za kimaendeleo Wilaya.**
Katika Wilaya ya Micheweni Miradi ya ujenzi wa barabara Kiuyu Maziwa Ngombe, Mradi wa eneo la uwekezaji maziwa ngombe, mradi wa kituo cha afya Shumba Mjini, bandari ya shumba mjini, Hospital ya Micheweni, Mradi wa Ujenzi wa skuli ya Micheweni, mradi wa kisima kironjo, mradi wa bonde la ukele na

ujenzi wa nyumba za waliothirika wa maafa – Tumbe imeratibiwa na kutekelezwa.

*(d)* **Kutekeleza na kusimamia Mpango wa Taifa wa kupambana na udhalilishaji wa wanawake na watoto.**

Aidha, kwa upande wa ofisi ya wilaya, jumla ya matukio 11 ya udhalilishaji yameripotiwa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ndani ya kipindi cha miezi mitatu, ikiwemo utelekezaji 7 na mvutano wa malezi 4. Katika utekelezaji wa mashauri hayo: mashauri 6 ya utelekezaji yameshapatiwa ufumbuzi na moja ipo katika hatua za utatuzi na mashauri 3 ya mvutano wa malezi yameshapatiwa ufumbuzi na moja lipo katika hatua ya utatuzi.

***Miakakati iliyojiwekea Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Micheweni.***

Ofisi imeweza kujiwekea mikakati mbali mbali katika kufikia hatua ya maendeleo, mikakati hiyo inajumuisha mambo yafuatayo:-

*(a)* Kusimamia na kuimarisha ulinzi na usalama katika Wilaya kwa kutoa elimu ya uraia kwa wananchi ili kudhibiti wahamiaji haramu.

*(b)* Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa kijinsia kwa kuendelela kutoa elimu kwa jamii juu ya athari ya vitendo hivyo pamoja na kuzijengea uwezo Kamati za Hifadhi ya Mtoto za Shehia.

*(c)* Kudhibiti Uingiaji na utokaji wa madawa ya kulevya na wageni kupitia Bandari bubu zilizomo ndani ya Wilaya.

*(d)* Kufanya doria za mara kwa mara kudhibiti vitendo viovu.

*(e)* Kudhibiti athari mbaya za Usalama barabarani ndani ya Wilaya ya Micheweni.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA WILAYA MICHEWENI**

Katika utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Kamati imebaini changamoto nyingi ambazo ni kikwazo cha ufanisi wa shughili zao, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatavyo :-

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa kiwango kikubwa cha kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto ambazo husuluhishwa

kupitia vikao vya wazee wa Mji, jambo ambalo huongeza kasi ya kasi hizi kwa vile hazipatiwi hatua sahihi za udhibiti.

*(ii)* Kamati pia, imebaini kuwepokwa uhaba wa vitendea kazi vya ofisi pamoja na vyombo vya usafiri kwa maafisa mbali mbali ambao wanatoa huduma katika jamii, matokeo yake ni kushindwa kuifikia jamii na kuwapa elimu juu ya masuala mtambuka.

*(iii)* Kamati pia, imebaini kuwepo kwa mwamko mdogo wa jamii zinazoishi pembezoni mwa bahari katika masomo ya skuli na madrasa za Qurani.

**MAONI USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Serikali ya Wilaya kuwachukulia hatua wazazi na walezi ambao wanaficha na kutoa suluhu ya kesi za udhalilishaji hivyo, kuongeza kasi ya ongezeko la kesi hizi.

*(ii)* Uogozi wa Wilaya uandae mpango maalumu utakaozisaidia Taasisi za Serikali kupata vifaa vya kutosha katika utendaji wao ili kupata ufanisi wa kazi zao.

*(iii)* Ofisi ya Wilaya kupitia Radio Jamii iongeze kasi ya kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kusimamia watoto kupata elimu bora pamoja na elimu ya mazingira kwa lengo la kujikwamua adui njaa na ujinga.

## 3.26 BARAZA LA MJI WETE

Baraza la Mji Wete ni miongoni mwa Serikali za mitaa ambazo utendaji wake umekuwa ukikua siku hadi siku kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha kwa kipindi kifupi cha miezi mitatu Baraza lilijipangia kutekeleza program kuu moja ikiwa ni Usimamizi na Uendeshaji wa Baraza la Mji Wete. Programu hiyo ikiambatana na utekelezaji wa progamu ndogo tatu ambazo ni;

a) Mipango, fedha na Utawala
b) Uratibu wa masuala ya mtambuka
c) Ustawi wa jamii Kiuchumi

**Utekelezaji wa Baraza la Mji Wete:**

***(a)* Kuimarisha huduma za Mipango, fedha na rasilimali watu;**
Kupitia programu kuu ya Usimamizi na uendeshaji wa Baraza la Mji Wete, Baraza limeweza kununua vitendea kazi vikiwemo vifaa vya kuandikia, vifaa vya kufanyia usafi, upatikanaji wa huduma za mawasilino ya ofisi ikiwemo vifurushi vya POS mashine, kulipa mishahara, stahiki za watumishi na Waheshimiwa madiwani.

***(b)* Kuimarisha huduma za jamii na usafi wa mazingira;**
Katika uimarishaji usafi maeneo ya Mji wa Wete na kuupendezesha mji, Baraza limefanikiwa kukusanya jumla ya tani 630 za taka ngumu na kusafisha misingi ya maji machafu yenye urefu wa kilomita 8.0 Ofisi inaendelea na mkakati wa kudumisha usafi wa mazingira kila Jumamosi kwa kushirikiana na Wananchi Katika kuimarisha huduma za Jamii Ofisi imejenga Slabu nne4 za kuhifadhia taka katika maeneo ya Kifumbikai, Limbani, Selemu na Kizimbani na jumla ya Shs 14,000,000/= zimetumika.

***(c)* Kuyawezesha makundi maalum kuimarika kiuchumi;**
Kupitia program ya kuwawezesha wajasiriamali kiuchumi na kusaidia makundi maalum kuimarika kiuchumi Ofisi imetenga jumla ya T.Shs 10,000,000/= kutumika kwa lengo la kuwasaidia walengwa.

***(d)* Utekelezaji Wa Shughuli Za Maendeleo;**
Jumla ya T.Shs14,000,000/- zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya jamii ambapo jumla ya Slabu nne za kuhifadhia taka zimejengwa katika maeneo ya Limbani, Kifumbikai, Selemu na Kizimbani fedha hizo zilitumika katika mchanganuo ufatao T.shs. 11,565,217 zimetumika kwa utekelezaji wa mradi, T.Shs 608,696/- malipo ya TRA na T.Shs1,826,087 ni malipo ya ZRB.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BARAZA LA MJI WETE**

Afisi ya Baraza la Mji Wete inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo: -

*(i)* Changamoto kubwa ya uchache wa vyombo vya Usafiri hasa gari ya kubebea taka na ya ufuatiliaji;

*(ii)* Kamati pia, imebaini kuwepo kwa uhaba wa wataalamu wa mapato ambao watatumika kukusanya lakini pia kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa mujibu wa wakati tulionao.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Kamati inalishauri Baraza la Mji Wete kuandaa mpango maalumu utakaowawezesha kupata vyombo vya usafiri ikiwa ni pamoja na kuwatumia wataalamu katika kuandaa miradi ya kimaendeleo kupitia nchi Wahisani na Taasisi za Fedha.

*(ii)* Kamati inashauri Baraza kufanya tathmini ya kina juu ya vyanzo vyake vya mapato na kupata taarifa kaamili juu yaongezeko au anguko la mapato kupitia vyanzo vyake. Vile vile, Baraza libuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza kasi ya ukusanyaji.

## 3.26 HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI

**Utekelezaji halisiwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa:**

***(a)*** **Mapato na matumizi kwa kipindi cha Julai-Septemba 2021;**
Katika kuongeza nguvu na ufanisi kwenye ukusanyaji wa mapato, Halmashauri ilikadiria kukusanya T.Shs 84,482,500/= kwa kipindi cha Julai-Septemba, hadi kufikia 30 Septemba, imefanikiwa kukusanya T.Shs 71,384,206/= sawa na asilimia 84.49 ya makadirio. Ambapo fedha hizo zilitumika katika shughuli za uendeshaji na za maendeleo.

***(b)*** **Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo;**
Katika kusimamia na kuratibu mipango na miradi ya maendeleo, Halmashauri kwa kipindi cha Julai-Septemba, 2021 ilipanga kufanya maandalizi ya ujenzi wa kituo cha Daladala cha Konde na imefanikiwa kukamilisha taratibu za awali za upatikanaji wa eneo la ujenzi wa Kituo cha daladala, kuandaa BOQ pamoja na Mchoro wa Mradi huo.

***(c)*** **Kuyawezesha Makundi Maalumu kujiimarisha Kiuchumi;**

Katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, Halmashauri imefanikiwa kutenga Jumla ya Shs 9,250,000/= ambayo ni sehemu ya asilimia 10 ya makusanyo kwa ajili ya makundi hayo.

***(d)*** **Kuimarisha usafi wa mazingira;**
Katika kuimarisha usafi wa mazingira kwenye maeneo ya miji, fukwe, barabara, misingi ya maji ya mvua na masoko, Halmashauri imefanikiwa kukusanya tani za taka ngumu 350 na kutupwa sehemu husika, mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 460 kwa kila mwezi ilisafishwa katika maeneo ya Konde, Sizini na Mapofu.

***Mikakatiiliyojiwekea Halmashauri ya Wialaya ya Micheweni*;**
Afisi ya Halmashauri ya Wialaya Micheweni imejipangia mikakati kadhaa katika utekelezaji wake, miongoni mwa mikakati hiyo ni kama ifatayo: -

***(a)*** Kuendeleza wigo wa udhibiti wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya electronic na Kubuni vianzio vipya vya mapato.
***(b)*** Kutoa elimu kwa jamii juu ya utunzaji, usafishaji na udhibiti wa mazingira na ulipaji wa kodi kwa hiari.
***(c)*** Kuandaa siku maalumu ya usafi kwa watumishi wote wa Wilaya kwa kila mwezi.
***(d)*** Kutoa elimu kwa Wajasiriamali juu ya umuhimu wa kujisajili.
***(e)*** Kutoa huduma bora kwa wananchi na kwa wakati.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI**

Katika utekelzaji wa majukumu yake ya kila siku, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(i)* Kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo.
*(ii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri kama vile magari, piki piki na vespa.
*(iii)* Uhaba wa vifaa vya kufanyia usafi kama vile magari ya kubebea taka.

*(iv)* Ucheleweshwaji wa mgao wa makusanyo ya fedha za maliasili zisizorejesheka kama vile, mchanga, mawe, kokoto, Kifusi na matofali.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Kamati inashauri Halmashauri kusimia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyake ili kusaidia ongezeko la iradi ya maendeleo.

*(ii)* Kamat inashauri Halmashauri kuyafikia moja kwa moja makundi maalumu ili kujua uwezo wao wa kiuchumi na kuyawezesha zaidi.

*(iii)* Halmashauri izidishe kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kuwatumia wataalamu wa mapato pamoja na kitafuta vyanzo vipya vitakavyo wasaidia kuongeza mapato.

*(iv)* Halmshauri ihakikishe imeziba mianya ya mapato na kutoruhusu matumizi holela ya rasiliamali zilizomo ndani ya Halmashauri yao.

*(v)* Kamati pia, inashauri Halmashauri kuzidisha kazi ya ujenzi wa kituo daladala cha Konde ili kuongeza vyanzo vya mapato.

## 3.27 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, nambari *3* ya mwaka *2018*.

Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imeendelea kutekeleza majukumu yake kama Ofisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinavyosimamia na kuratibu kazi za Serrikali. Ofisi hii inatoa huduma kwa Wananchi kwa kufuata miongozo ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma Zanzibar.

***Majukumu yanayotekelezwa na Wakala wa usajili wa matokeo ya kijamii.***

*(a)* Kusajili wenye sifa ya Uzanzibar Mkaazi
*(b)* Kutoa Vitambulisho kwa watu ambao wameshasajiliwa.
*(c)* Kufanya uboreshaji (Update) wa taarifa za Wananchi.
*(d)* Kusajili Vizazi na Vifo.
*(e)* Kutoa Vyeti vya kuzaliwa pamoja na Vyeti vya Vifo.

*(f)* Kukusanya Mapato yatokanayo na Usajili wa Vyeti vya kuzaliwa,
*(g)* Vyeti vya ndoa, Vyeti vya Vifo na upoteaji wa Vitambulisho.

**Utekelezaji halisi wa shughuli zilizopangwa na ZCSR-Pemba:**

- ***Hali ya usajili kwa kipindi cha Julai-Septemba 2021.***
  Katika kutoa huduma ya Usajili Pemba kwa kipindi cha Julai-Septemba, Ofisi imefanikiwa kusajili jumla ya Vizazi **5423**, jumla ya wananchi **3594** walijisajili kwa ajili ya kupata Vitambulisho, jumla ya matokeo **344** ya vifo na vizazi yaliripotiwa, jumla ya Wananchi **4900** wamechukuwa Vitambulisho vyao kwa Wilaya zote nne(4) za Pemba.

- ***Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Jualai-Septemba 2021 kwa upande wa Pemba:***
  Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki ni ni kama yafuatayo:-

  *i.* Ofisi imefunga mifumo mipya ya Usajili wa Vyeti kwa njia ya kisasa (dijitali) na kuanza kuitumia.

  *ii.* Ofisi imefanikiwa kuwa na uwezo wa kuingizwa taarifa katika mfumo na kuweza kutoa Vyeti kwa wahusika kwa njia ya haraka na kupunguza usumbufu kwa wananchi.

  *iii.* Ofisi imeweza kupata Mashine zenye uzito mwepesi sana (Mobile machines) kwa ajili ya ugawaji wa Vitambulisho mpaka kwenye Shehia bila usumbufu.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WAKALA WA USAJILI WA MATOKEO YA KIJAMII ZANZIBAR:**

Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii inakabiliwa na Changamoto zifuatazo:-

*(i)* Upungufu wa Wafanyakazi katika kada mbali mbali kama vile Afisa Mipango, Masjala Bayana, Muangalizi wa Afisi, MtunzaGhala (StoreKeaper), Mkaguzi wa ndani, Kalamazuu na Muhudumu, Wasaidizi Maafisa wa Wilaya kwa Wilaya tatu za Pemba Wilaya Wete, Wilaya Micheweni, Wilaya Mkoani.

*(ii)* Afisi pia inakabiliwa na changamoto ya vyombo vya usafiri ambapo husababisha baadhi ya vituo kushindwa kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi wakati wa kutoa huduma vijijini.

*(iii)* Wakala inakabiliwa na changamoto ya Ofisi kwa uppande wa Pemba, kwa sasa ofisi inayotumika kama makao makuu ya Pemba uwezo wake ni mdogo na hulazimika chumba kimoja cha ofisi kutumiwa na watu zaidi ya wawili wenye kada tofauti. Hata hivyo, mandhari yanofisi yenyewe hairidhishi kwa kuzingatia usalama wa kiafya kutokana na ufinyu mkubwa wa nafasi.

*(iv)* Kuwepo kwa kiwango kikubwa cha wananchi wanaosajili vyeti baada ya kupitiwa na muda (late registration). Kamati imebaini katika vituo kadhaa vya usajili ipo changamoto hii na hivyo kuwataka wananchi wajisajili mara tu wanapojifungua.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Katika kuleta mustakbali uliobora wenye ufanisi na tija kwa jamii, Kamati inashauri jamii kubadilika kulingana na wakati tulionao kwa kufanya usajili wa matukio mbali mbali kwa wakati na kwa kutoa taarifa zilizosahihi.

*(ii)* Kamati inaishauri Serikali kuzidi kuziboresha ofisi za usajili wa matukio wilayani ili wananchi wapatiwe huduma za uhakika na wakati.

*(iii)* Aidha, Kamati inashauri elimu izidi kutolewa kwa jamii juu ya umuhimu wa kujisajili na kuchukua vyeti na vitambulisho vyao kwa wakati.

## 3.0 OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilirejea rasmi mwezi wa *Disemba, 2020* ambapo inashughulika na masuala mtambuka ya uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira, masuala ya watu wenye ulemavu, masuala ya VVU na UKIMWI na masuala yanayohusu udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha, Ofisi hii inasimamia na kuratibu Ofisi ya faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais, pamoja na masuala ya Sera, Mipango na Tafiti za Ofisi.

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaundwa na Idara zifuatazo:

*(a)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(b)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
*(c)* Idara ya Mazingira.
*(d)* Mamlaka ya Mazingira Zanzibar.
*(e)* Idara ya Watu Wenye Ulemavu.
*(f)* Ofisi ya Faragha.
*(g)* Ofisi Kuu Pemba.

## 4.1 IDARA YA MAZINGIRA ZANZIBAR.

Idara ya Mazingira ni miongoni mwa taasisi zilizomo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo jukumu lake kubwa ni kuhakikisha kuwa nyenzo za usimamizi wa mazingira (environmental management tools) ikiwa ni pamoja na sera, sheria, Kanuni, mikakati na miongozo inakuwepo; kutoa elimu ya Mazingira kwa jamii pamoja na kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi Zanzibar.

Kazi za Idara ya Mazingira ni kazi ambazo amepewa Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika kifungu cha 13 cha Sheria Namba 3 ya mwaka 2015.

## 4.2 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR (ZEMA)

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) imeanzishwa mwaka 2015 chini ya kifungu cha 14 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ya mwaka 2015. Lengo Kuu la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ni kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria, kanuni, miongozo na viwango vya mazingira kwa ajili ya kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Mamlaka hii itasimamiwa na Bodi iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015. ZEMA imepangiwa majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015.

## 4.3 PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Programu hii inatekelezwa na Taasisi zote zinazosimaia masula ya kimazingira Zanzibar ikiwemo ZEMA ambapo utekelezaji upo kwa mujibu wa sharia ya Taasi husika. Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa programu hii kwa vipindi tofauti ambapo nguvu zaidi inahitajika katika kufikia malengo yaliyopangwa.

Kamati inapongeza juhudi zinazochukuliwa katika mapambano dhidi ya uhifadhi wa mazingira kwa kutekelezwa miradi mbali mbali ikiwemo mradi wa ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji chumvi kuvamia makaazi ya watu Msuka Wilaya ya Micheweni, mradi ambao mpaka sasa umefanikiwa kwa asilimia 90%.

**CHANGAMOTO YA UTEKELZAJI WA PROGARAMU:**

Changamoto kubwa ziliopo zinazohusiana na Sera, Sheria na mifumo ya kitaasisi katika Usimamizi wa mazingira, miongoni mwao ni kama zifuatavyo:-

*(i)* Muingiliano wa baadhi ya sheria ziliopo juu ya usimamizi bora wa sheria ambaokwa baadhi ya maeneo hautoi wajibu wa moja kwa moja kwa taasisi husika hasa kwenye suala la uharibifu na uchafuzi wa mazingira ya baharini.

*(ii)* Taasisi nyingi zinazohusiana na usimamizi wa mazingira na maliasili hazina uwezo mkubwa wa vifaa na teknolojia bora kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji na wa mazingira.

*(iii)* Mgongano wa kiutendaji na taasisi nyengine katika kusimamia na kutekeleza masuala ya mazingira imekuwa ukitoa fursa kwa wananchi kuendelea kuyaharibu mazingira.

*(iv)* Kuwepo kwa mazingira duni ya ufanyajikazi kwa Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira pia inarudisha nyuma juhudi za mampambano dhidi ya uhifadhi wa mazingira.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

*(i)* Kufanya mapitio ya Sheria za Mazingira ili kuondoa muingiliano wa majukumu wa baadhi ya sheria zilizopo juu ya usimamizi wa mazingira.

*(ii)* Kufanyiwa mapitio ya Sheria nyengine zinazohusiana na mazingira kama vile Sheria ya misitu, Sheria ya usafiri baharini; na kutunga sheria mpya ya Madini itakayojumuisha pamoja na mambo mengine ya usimamizi wa maliasili zisizorejesheka.

*(iii)*Kuimarisha upatikanaji wa vifaa, teknolojia bora na wataalamu wa usimamizi wa mazingira kwa lengo la kuimarisha mikakati endelevu ya usimamizi wa Mazingira.

*(iv)*Tafiti zaidi zinahitajika juu ya nishati mbadala ya kuni na mkaa katika matumizi ya kupikia ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wa kipato cha chini.

*(v)* Serikali izidishe kasi ya mapambano dhidi ya uingizaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki kwa Taasisi zinzohusika kuwachukulia hatua za kisheria wahusika.

*(vi)*Serikali isimamie maeneo yaliyoathirika na uchimbaji wa mchanga ili kurudishwa katika hali ya asili kwa kuhakikisha maeneo hayo yamepandwa miti ina imekuwa.

*(vii)* Kamati inasikitishwa na tabia za watu kuona kwamba sula la uhifadhi wa mazingira ni la Serikali pekee ilahli ni suala mtambuka ambalo kila mmoja anapswa kulichukulia hatua. Hivyo, jamii ishirikishwe moja kwa moja katika mapambano dhidi ya uhifadhi mazingira kwa kupewa elimu ya kuhifadhi mazingira.

*(viii)* Jitahada za makusudi zinahitaji katika kuviokoa visiwa vidogo vidogo kutokana na mabadiliko ya Tabianchi. Hivyo, Serikali inapaswa kuweka mikakati maalumu itakayowashirikisha wenyeji wa visiwa hivyo dhidi ya mpango wa kuhiofadhi mazingira.

## 4.4 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

### 4.4.1 TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya, nam. *12* ya mwaka *2011* ambayo inasomwa pamoja na Sheria nambari *9* ya mwaka *2009*. Majukumu ya Tume hii yameainishwa katika kifungu cha *5* cha Sheria hiyo.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KUPITITIA UTEKELEZAJI:**

*(a)* Ofisi imekamilisha utaratibu wa kufuta na kuunda sheria mpya ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya itakayopelekea kuunda Mamlaka itakayokua na nguvu ya kisheria kupambana na masuala ya Dawa za kulevya. Sharia mpya ya kufuta Sheria Namba 9/2009 tayari imeshapitishwa na mabadiliko ya Sheria hiyo yataongeza ufanisi kwa kiasi kikubwa katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevya hapa Zanzibar.

*(b)* Rasimu ya muundo mpya wa taasisi itakayopelekea Tume ya Uratibu wa Dawa za Kulevya kuwa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar tayari imeshaandaliwa na kuwasilishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa hatua zinazofaa ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sharia yake.

*(c)* Katika kupunguza usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya, operesheni 42 zilifanyika katika mitaa iliyobainika kuwa ni hatarishi zaidi kwa kipindi cha July – Septemba, 2021. Mitaa hiyo ni Kinuni, Mtoni Kidatu, Jango’ombe, Nyerere, Makunduchi, Rahaleo, Mwembeladu, Mjimkongwe, Fuoni, Kidongo chekundu, Bububu, Mboriborini, Mangapwani, Bumbwini, Kihinani, Migombani na Darajabovu. Pia, doria za mara kwa mara zimeendelea kufanyika na kupelekea kupunguza matumizi na biashara ya dawa za kulevya mitaani na kuimarisha mashirikiano baina ya wananchi na Serikali katika kupunguza wimbi la usambazaji wa dawa za kulevya.

*(d)* Ofisi imeanzisha huduma ya simu ya bure kupitia namba 0774 33 33 00 kwa ajili ya kuripoti taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya. Hadi kufikia Septemba 2021 simu 37 zimepokelewa zikitoa taarifa

za uhalifu kwa usiri na kwa haraka, jambo ambalo limerejesha imani kwa wananchi katika kutoa taarifa za uhalifu wa Dawa za Kulevya.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TUME**

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa ukosefu wa vifaa vya kisasa vya utambuzi wa dawa za kulevya katika viwanja vya ndege na bandari zetu za Unguja na Pemba pamoja na uhaba wa GPS zitakazosaidia kugundua maeneo yenye wahalifu.

*(ii)* Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la uhaba wa ofisi za kisasa za Tume zenye majengo yanayoendana na hali halisi ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya, sambamba na uhaba wa rasilimali watu ambao ni kiungo muhimu katika kuiwezesha Tume kiutendaji.

*(iii)* Kamati pia imebaini kuwepo kwa changamoto ya kucheleweshwa kwa kesi za madawa katika kutolewa hukumu hivyo, kuwafanya wahalifu kujipanga na kuziharibu kesi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMAMATI**

Kutokana na changamoto kadhaa ambazo wanakabiliana nazo katika mazingiira mbali mbali, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

*(i)* Mazungumzo na Washirika wa maendeleo yenye lengo la kuipatia ofisi kifaa cha kisasa “body screen” yanaendelee ili kuisadia Tume kwenda na wakati. Kifaa hicho kitakapopatikana ni vyema kufungwa katika Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Unguja. Aidha, Ofisi izingatie suala la ununuzi wa kifaa cha GPS kupitia Bajeti yake ya mwaka wa fedha unaofuata.

*(ii)* Mashirikiano zaidi yajengwe baina ya jamii na Tume ili kusaidia kupata taarifa za kudhibiti bandari bubu ambazo inasemekana kwa kiasi kikubwa zinatumika kupitishia dawa za kulevya.

*(iii)* Pia, ifikie pahala Mahakama iwe na idara maalumu ambayo itashughulikia kesi za Dawa za Kulevya pekee kama ilivyo kwa kesi za udhalilishaji ili kuziwezesha kesi kwenda kwa haraka.

(*iv*) Tume iandae mpango maalum utakaowawezesha kutoa zawadi kwa wananchi wanaotoa taarifa za dawa za kulevya pamoja na kuzidisha operesheni za uchunguzi katika ngazi ya vijiji na shehia.

(*v*) Vile vile, Serikali ifikirie zaidi umuhimu wa kuboresha maslahi ya watendaji wa Tume ili kuwadhibiti kutoshiriki katika vitendo vya rushwa na uhujumi wa uchumi kupia kadhia hii ya dawa za kulevya.

## 4.5 TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Tume ya Ukimwi Zanzibar imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Ukimwi, nam. *3* ya mwaka *2002* ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kuhakikisha kuwa Mikakati ya Kitaifa, Sera na Miongozo itakayoongoza mapambano dhidi ya Virusi vya *UKIMWI* na *UKIMWI* inaandaliwa pamoja na kupunguza makali ya virusi vya *UKIMWI* na *UKIMWI* kwa kuhamasishana kuratibu utekelezaji wa Sera na Mikakati hiyo.

### 4.5.1 PROGRAMU YA KURATIBU MUITIKO WA TAIFA WA UKIMWI

Mfanikio yaliyopatikana kupitia programu ya kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI ni kama ifuatavyo:-

(*a*) Ofisi imefanya mkutano na asasi 34 zinazopambana na UKIMWI kwa lengo la kuzitambua na kufahamu uhalali wa kuanzishwa kwake pamoja na kuwapatia miongozo mbalimbali ikiwemo kuandaa mipango kazi katika kutekeleza shughuli za ukimwi. Asasi zilizoshiriki ni Zapha+, ZYF, RCZ, ZANPUD, YOSEFO, SAOA, ODYDO, BIO, ZANA, DFZ, ZACA, YOSOA, CHUYODO, ZASO, AMREF na UMATI.

(*b*) Ofisi imefanya ufuatiliaji kwa Unguja na Pemba katika taasisi 11 na mashirika ya Umma mawili kwa lengo la kuangalia ni kwa kiasi gani masuala ya UKIMWI yanazingatiwa katika utekelezaji wa miradi mikubwa. Katika ufatiliaji huo, ilibainika kuwa sekta nyingi hazizingatii kipengele cha masuala ya UKIMWI katika miradi mikubwa ya maendeleo. Miradi mingi imeonekana kuratibiwa Unguja katika Ofisi kuu za sekta hizo na Pemba kutekeleza sehemu tu ya miradi hiyo. Aidha, waratibu na wasimamizi wa

miradi hiyo wameonekana kuwa na uelewa mdogo juu ya umuhimu wa kuingiza kipengele hicho.

*(c)* Ofisi pia kwa kipindi cha kota ya mwanzo Bajeti, imeratibu programu za ujumuishaji wa huduma za UKIMWI kwa kufanya ziara za ufuatiliaji katika kliniki za tiba 12 na vituo rafiki kwa vijana 13 Unguja na Pemba. Ziara hizo zimefanyika kwa lengo la kuiwezesha jamii kupata huduma kwa urahisi na kuokoa muda wa kufuata huduma sehemu tofauti. Jumla ya wanawake 90 wanaoishi na VVU wamepatiwa huduma za uzazi wa mpango kupitia kliniki za tiba. Wanawake 619 wamepimwa saratani ya shingo ya kizazi na watu 6,265 wamefanyiwa uchunguzi wa maradhi ya kujamiiana. Aidha, vijana 2,588 walipatiwa huduma katika vituo rafiki ikiwemo upimaji wa VVU ambapo vijana 1,434 walipima VVU na saba waligundulika kuwa na VVU wakiwemo wanaume wawili na wanawake watano.

*(d)* Ofisi imetoa mafunzo kwa watoa huduma 20 kutoka vituo vya afya vinavyotoa huduma za UKIMWI na afya ya uzazi kwa Pemba. Mafunzo hayo yalilenga utoaji wa huduma sahihi na uhamasishaji juu ya matumizi sahihi ya mipira ya kike na kiume ili kupunguza maambukizo ya VVU kwenye jamii.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA TUME YA UKIMWI**

Licha ya mafanikio kadhaa ambayo yametikana katika vipindi tofauti vya maisha ya Tume ya UKIMWI kupitia programu ya kuratibu muitiko wa Tume ya UKIMWI, kumekuwepo changamoto kadhaa ambazo zinaathiri maendeleo ya Tume katika mapambano dhidi ya janga la UKIMWI. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

*(i)* Kamati imebaini kwamba maradhi ya UKIMWI sasa yanaonekana si tatizo tena katika jamii ilihali bado ni tatizo na linaitekeza jamii kwa kiasi kikubwa na kupunguza nguvu kazi ya jamii.

*(ii)* Kamati pia, imebaini mapambano dhidi ya maradhi ya UKIMWI yanatumika kama ni fursa ya kujipatia kipato badala ya kufanywa ni njia ya kutokomeza maradhi haya kutokana na kuanzishwa kwa jumuiya kadhaa ambazo zinahusika na mapambano ya UKIMWI ilhali ongezeko ni kubwa na jamii inaathirika.

*(iii)* Kamati imebaini kuwepo kwa ongezeko kubwa la biashara ya ngono katika maeneo mbali mbali ya miji yetu kwa Unguja na

Pemba jambo linaloongeza kwa kasi zaidi maradhi ya UKIMWI na maradhi mengine ya uasharati katika jamii.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Kupitia changamoto hizi, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

*(i)* Takwimu za hali halisi ya maradhi ya UKIMWI ziendelee kutolewa pamoja na elimu katika jamii kupitia ngazi ya Wilaya na Mkoa. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na NGO's ziendelee kutoa uelewa na kuihamasisha jamii kupitia mitandao ya kijamii, Redio, Televisheni na mikutano juu ya uwepo wa maradhi ya UKIMWI na athari zake kwa jamii na uchumi kwa ujumla.

*(ii)* Mapambano dhidi ya UKIMWI yasitumike kama fursa ya kujipatia kipato katika jamii bali yafanyike kama njia ya kupunguza maambukizi na athari za maradhi haya katika nchi yetu. Kufanya hivyo kutasaidia kufikiwa lengo lililokusudiwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

*(iii)* Serikali iiwezeshe Tume ya UKIMWI Pemba kwa kuwapatia ofisi bora yenye uwezo wa kutoa huduma kwa jamii pamoja na kuboreshwa kwa sekta usafiri ili kurahisisha kazi zao za kutoa elimu na mapambano ndhidi ya VVU.

*(iv)* Serikali iandae mkakati maalumu utakao komesha biashara haramu ya ngono katika nchi yetu. Aidha, jamii ifahamu kwamba mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ni jukumu la kila mmoja, hivyo ni wajibu wetu kuyaendeleza mapambano kwa kutojihusisha na vitendo vitakavyopelekea ongezeko la maambukizi mapya.

## 4.0 OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi imeanzishwa mwaka *2010* kutokana na mabadiliko ya *kumi na moja (11)* ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* toleo la *2010*. Jukumu kuu la msingi la Wizara hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na masuala ya Muungano kwa upande wa Zanzibar. Aidha, majukumu makhsusi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi ni pamoja na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais; kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa; kuandaa na kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa; kuratibu masuala ya Muungano; kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara. Vilevile, inaratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Wawakilishi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Aidha, Wizara hii inaundwa na Idara zifuatazo:

*(i)* Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais.
*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(iii)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
*(iv)* Idara ya Maafa.
*(v)* Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.
*(vi)* Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali.
*(vii)* Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ.
*(viii)* Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

Vile vile, Wizara hii inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

*(i)* Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.
*(ii)* Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

### 4.1 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

### 4.2 BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni miongoni mwa mihimili *mitatu (3)* ya Serikali ambapo lilianzishwa kwa ajili yakustawisha demokrasia na uwakilishi wa watu wa Zanzibar. Majukumu makuu

ya Baraza ni kutunga sheria, uwakilishi wa wananchi na usimamizi wa Serikali.

Baraza katika kazi zake za usimamizi linajumuisha usimamizi wa fedha za umma, mapato na matumizi ambayo yaliidhinishwa na Baraza.

## 4.3 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Tume ya Uchaguzi Zanzibar ni chombo kilichoanzishwa mwaka *1979* chini ya kifungu cha *73* cha Katiba ya Zanzibar ya *1979*. Kwa hivi sasa Tume ya Uchaguzi Zanzibar inafanya kazi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya *1984*, Sheria ya Kuanzishwa kwa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, nam. 1 ya *2017*, Sheria ya Uchaguzi, nam. *4* ya *2018* na Sheria ya Kura ya Maoni, nam. *6* ya *2010*. Miongoni mwa majukumu makuu ya Tume ni kukuza na kusimamia mienendo ya uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

## 4.4 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (III)

TASAF ni chaombo muhimu ambacho kiliundwa kwa mashirikiano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kupambana na umasikini. Chombo hiki kinaendesha shughuli za usimamizi wa miradi kupitia ufadhili wa Washirika wa Maendeleo wakiwemo World Bank, UNDP, DFID, UNICEF pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Katika utekelzaji wa TASAF (III) Kamati imeridhishwa na mikakati na miradi inayotekelzwa kwa lengo kupunguza umasikini. Kwa upande wa Pemba Kamati ilifanikiwa kutembelea mradi mkubwa wa ujenzi wa Kituo cha afya, wodi ya wazazi na nyumba ya Daktari katika Shehia ya Kendwa, Wilaya ya Mkoani.

Aidha, Kamati imetembelea miradi inayotekelezwa kupitia Kaya Masikini na kupata kuzungumza nao kwa lengo la kutathmini mafanikio yanayopatikana kupitia miradi ya TASAF.

## MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KUU

Mafanikio yafuatayo yamepatikana kutokana na utekelezaji wa programu hii:

*(a)* Kuimarika kwa hali za kiuchumi za walengwa kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini TASAF na kupungua malalamiko ya walengwa mabao walitolewa kimakosa katika mfumo wa malipo.

*(b)* Kufanya uhaulishaji wa fedha kwa kaya masikini 13,610 katika Shehia 78 zilizomo katika mpango, Pemba ambapo jumla ya Shilingi Milioni 7.15 zilizopangwa zililipwa kwa walengwa.

*(c)* Kufanywa uhakikiwa walengwa ambao walikuwa hawapokei malipo kutokana na kutolewa kimakosa katika mfumo wakati wa uhakiki wa awali wa walengwa. Jumla ya walengwa walihakikiwa na kulipwa malipo ya kawaida na malimbikizo yao.

*(d)* Kwa upande wa kisiwani Pemba, jumla ya miradi 74 ya kutoa ajira za muda katika Shehia 69 zilizomo katika mpango zilinufaika kwa asilimia 70 kupitia sekta ya kilimo, Mazingira, barabara, misitu na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

**CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

Utekelezaji wa programu kuu hii unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*1.* Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya kuchelewa kwa fedha za miradi ya TASAF kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini.

*2.* Kuwepo kwa baadhi ya walengwa ambao wametolewa kimakosa katika mfumo na hivyo kusababisha malalamiko katika jamii.

*3.* Njia zinazotumika kupata walengwa wa kaya masikini zinachangamoto hivyo kupelekea baadhi ya wanajamii wenye mazingira magumu ya maisha kushindwa kuingizwa katika mfumo nakuwa wanufaika wa mradi huu.

*4.* Baadhi ya wanajamii hawatoi taarifa sahihi wanaposajiliwa au kuhakikiwa na hivyo kupelekea kuwepo kwa taarifa zisizosahihi, athari yake ni kutolewa katika mfumo au kupata fedha tofauti na matarajio.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

Kamati, inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo juu ya utekelezaji wa programu kuu:

1. Kamati inatoa shukurani za dhati kwa watendaji wote wa TASAF pamoja na Makao Makuu yake kwa kuetekeleza vyema malengo ya mradi huu katika jamii.

2. Kamati inashauri TASAF kuanzisha ofisi ndogo Zanzibar kama ilivyo kwa Miradi/Taasisi nyengine za Tanzania Bara ili kutatua baadhi ya changamoto zake bila ya kutegemea Makao Makuu.

3. Wizara ifanye utafiti kwa lengo kufahamu kwa namna gani Zanzibar ilinufaika kupitia TASAF (II) na mapungufu yatakobainika yachukuliwe hatua za maboresho katika Phase III.

4. Kamati inashauri miradi ya barabara inayotekelezwa kupitia kaya masikini ifanyiwe utafiti kwa kutambua hasara na faida yake kupitia barabara zilizotengenezwa. Kamati inaona imefika wakati mpango wa matengenezo ya barabara kuondolewa katika mradi kupitia kaya masikini kwani hazina ufanisi na hivyo kusababisha changamoto zaidi kwa watumiaji wakati wa mvua.

# SEHEMU YA TATU

## 5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA JUMLA YA KAMATI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kipindi cha utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2021/2022 imeweza kufanya mizunguko yake katika kila *robo mwaka* kwa Taasisi zilizo chini ya Kamati hii na kutoa maoni, ushauri na maelekezo ambayo inatarajia yatawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku, hatua ambayo italeta manufaa kwa wananchi na Serikali kwa ujumla.

Kiujumla Kamati imeridhishwa na utendaji wa Taasisi zote ambazo zinasimamiwa na Kamati hii kutokana na juhudi zao kubwa wanazozichukua katika utekelezaji wa majukumu yao kufuata muongozo na taratibu za kisheria.

Hivyo, mbali ya maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa kwa kila Sekta, kamati pia inatoa maoni, ushauri na maelekezo ya jumla kwa Sekta hizo kama ifuatavyo:-

### 5.1 Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

(a) Serikali iangalie kwa kina upangaji wa watumishi kwa mujibu wa majukumu na nafasi zao katika taasisi zake kwa vile zipo baadhi ya taasisi zinalalamika kuwa na upungufu wa watumishi huku taasisi hizo zikiwa na watumishi wengi.

(b) Serikali izitumie Taasisi za kusimamia haki jinai kutoa elimu juu ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na changamoto zake kwa kesi za udhalilishaji katika jamii na athari yake katikam Nyanja za kiuchumi Kijamii na kisiasa.

### 5.2 Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

*(a)* Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalumu wa kuwalipa mishahara waheshimiwa Madiwani au maposho kutoka Serikali kuu badala ya kuwaachia wakurugenzi kuwalipa maposho, kufanya hivyo kutasaidia Madiwani kutekeleza vyema majukumu yao bila kuingiliwa na wakurugenzi.

(b) Serikali izisaidie Halmashauri zote kuanzisha mradi wa kuzalisha umeme wa gesi asilia na mbolea kama nishati mbadala katika kutunza mazingira kwa kuepusha kutumia kuni ambazo zinapelekea ukatwaji wa miti kwa kiwango kikubwa katika misitu iliyotuzunguka.

(c) Kamati inazishauri Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa kuhakikisha kwamba suala la ukusanyaji wa mapato, suala la usafi wa miji, malipo na stahiki za waheshimiwa Madiwani na wafanyakazi, miradi ya maendeleo, uhaba wa vitendea kazi na usajili wa wajasiriamali na wafanyabiashara wadod wado yamesimamiwa na kuchukuliwa hatua za moja kwa moja katika utekelezaji wake kwani haya ni miongoni mwa majukumu ya msingi katika Taasisi hizi.

(d) Kamati inashauri Vikosi vya Idara Maalumu za SMZ vipewe majukumu yake kwa mujibu wa Sheria zao, na kila kikosi kitekeleze wajibu wake kwa misingi ya sharia ya Idara husika.

(e) Kamati inashauri kila kikosi kijikite katika kakzi yake ya msingi pamoja na kuzalisha mali kwa lengo la kujitegemea pasina kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

(f) Kamati inashauri Serikali kuisimamia Taasisi inayohusika na kutoa Hati za umiliki wa Ardhi kuzipatia hati Idara zote ambazo zimeshakamilisha taratibu na kushindwa kuoatiwa hati zao. Kamati imebaini kwamba zipo baadhi ya Idara kama vile KVZ imekamilisha taratibu za malipo tokea mwaka 2011 na imekuwa ikikumbusha kila baada ya muda lakini hakuna utekelezaji wowote unaofanywa na Taasisi husika.

(g) Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri ambao utapunguza urasimu wa Sheria kwa vikosi vya Idara Maalumu wanapotekeleza miradi yao ya maendeleo. Kamati inasikitishwa na kuona zipo baadhi ya Taasisi ambazo zinahusika na miradi ya maendeleo zinakosa kutoa mashirikiano katika utekelezaji wa miradi ya vikosi.

## 5.3 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

(a) Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati maalumu utakaoviwezesha visiwa vidogo vidogo kuhifadhi mazingira na kuyalinda kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi

(b) Jamii pia ishajihishwe kupanda miti kwa wingi ili iwe ni njia mbadala ya kukabiliana na jana la mabadiliko ya tabianchi.

(c) Wizara ije na mkakatiu maalumu utakaofufua marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki kwani bado matumizi yanaendelea bila kuonekana juhudi kubwa zikichukuliwa na mamlaka husika.

**5.4 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi**

(a) Kamati inaishauri Serikali kuanzisha Ofisi ndogo ya Mfuko wa TASAF hapa Zanzibar ili iwe ni kimbilio na msaada wa wananchi katika kupeleka changamoto zao.

(b) Kamati inashauri miradi ya Kaya Masikini ifanywe kwa kuzingatia ubora na ufanisi wa mradi husika.

Aidha, Kamati inampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kusimamia vyema sera na mipango ya Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake za kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa upande mwengine, Kamati inatoa shukurani zake za dhati kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ndugu Raya Issa Msellem pamoja na wanasheria wetu wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa msaada wao mkubwa ambao wamekuwa wakiipatia Kamati hii wakati wa upitiaji wa Miswada ya Kisheria.

Aidha, pongezi maalum ziende kwa watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi pamoja na Afisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii, katika kipindi chote ambacho Kamati ilitekeleza majukumu yake na inawaomba waendelee kutoa ushirikiano na msaada wao wa dhati kila itakapohitajika.

=============== AHSANTENI==================